# Nipashe

Ijumaa Novemba 6, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580391

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710



TANESCO na ujenzi wa nyumba zetu

BUFE

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Hekaheka ya tabianchi ilivyokaribisha dhiki kwa wanakijiji wavuvi Mikuranga

UCHUMI

Mradi maji unaoibua uchumi wa kuzalisha vitunguu Babati

UKURASA 11

**KITENDAWILI** Spika, Naibu Spika Bunge kuteguliwa leo

UKURASA 3



**MNYUKANO** uenyekiti halmashauri waibua hisia kali Hai, Siha

UKURASA 4

# Magufuli ataja mambo muhimu

**NI** baada ya kuapishwa, aahidi mapambano zaidi ufisadi na rushwa, kuongeza makusanyo...*Endelea Uk. 2*



Dk. John Magufuli akiapishwa na Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma jana. Picha zaidi Uk. 19. **PICHA: IKULU**

## Trump maji ya shingo Marekani

UKURASA 3

## Museveni: Bila kujitegemea maendeleo Afrika ni ndoto

UKURASA 2


SALAMU ZA PONGEZI



Gazeti Nipashe linampongeza Rais Dkt John Magufuli na Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha Miaka 5. 2020 - 2025

Kwa salamu za pongezi
Wasiliana nasi kwa Simu: 0686 101335
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz



SALAMU ZA PONGEZI

HABARI KITAIFA

# JPM ataja maeneo ya vipaumbele

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS John Magufuli amekula kiapo cha kuwatumikia Watanzania kwa miaka mitano ijayo, huku akiainisha maeneo yatakayowekewa mkazo ikiwamo kuzidisha mapambano dhidi ya rushwa, wizi na ubadhirifu wa mali za umma.

Akizungumza jana na Watanzania katika Uwanja wa Jamhuri, mjini hapa baada ya kuapishwa, Rais Magufuli alisema uchaguzi sasa umekwisha jukumu kubwa lililopo ni kuendeleza jitihada za kulijenga na kuletea maendeleo taifa.

"Napenda niwahakikishie Watanzania wenzangu kuwa kiapo nilichoapa pamoja na alichoapa makamu wangu, tutahakikisha tunakienzi kwa nguvu zote. Tutashughulikia kero mbalimbali zinazowakabili wananchi wetu, tutazidisha mapambano dhidi ya rushwa, wizi na ubadhirifu wa mali za umma," alisema.

Pamoja na hayo alieleza kuwa wanalenga kukamilisha miradi mikubwa waliyoianzisha na kuanza kutekeleza mingine mipya.

"Vilevile, tutaimarisha usimamizi wa rasilimali zetu, ikiwamo madini, rasilimali za bahari, misitu, wanyamapori, mifugo, sambamba na hilo tutatekeleza kwa nguvu kubwa katika kukuza uchumi na kushughulikia kero ya umaskini, ukosefu wa ajira hususan kwa vijana," alisema.

Rais pia alisema atashirikiana na Watanzania katika kuendeleza jitihada za kujikomboa na kujenga taifa linalojitegemea bila kujali tofauti za kiitikadi, dini, kabila au rangi.

"Kama mjuavyo kwenye baadhi ya nchi uchaguzi umekuwa chanzo cha mifarakano, migogoro na vita. Sisi Watanzania kwa mara nyingine tumevuka mtihani huu salama na tumeuonyesha ulimwengu kwamba ni wapenda amani na tumekomaa kidemokrasia.

"Hii ni ishara nyingine kwamba Mwenyezi Mungu analipenda taifa letu. Tangu tumepata uhuru mwaka 1961, tumepita kwenye mtihani huu ambapo kwa mara zote tumevuka salama," alisema.

Kuhusu Dodoma, Magufuli alisema amekuwa Rais wa kwanza kuapishwa kwenye makao makuu ya nchi na kuahidi kuanza na ujenzi wa uwanja mkubwa wa michezo mkoani hapa.

Aliwashukuru wananchi kwa upendo wao ambao walianza kuingia usiku kwenye uwanja huo ili kupata fursa ya kushuhudia sherehe hizo.

"Ushindi tulioupata CCM umetokana na baraka zenu Wanadodoma, nawashukuru sana, napenda niwahakikishie yote tuliyoahidi wakati wa kampeni tutashughulikia ikiwamo kujenga barabara ya mzunguko ambapo sasa dalili zimeanza kuonekana kuwapo kwa msongamano Jiji la Dodoma," alisema.

Kadhalika, alishukuru viongozi wa mataifa mbalimbali waliohudhuria hafla hiyo na kueleza kuwa hiyo ni ishara nzuri ya mahusiano mazuri yaliyopo.

"Napenda niwahakikishie kuwa kama ilivyokuwa katika miaka mitano iliyopita, kwenye miaka mitano ijayo tutaendeleza zaidi na kukuza uhusiano, ushirikiano kati yetu na taasisi mnazowakilisha," alisema.

Magufuli alishukuru vyombo vya habari, vyombo vya ulinzi, wasanii kwa kufanya kazi kwa weledi wakati wote wa uchaguzi pamoja na Watanzania kwa kukipa ushindi mkubwa chama chake cha CCM.

Lakini kama nilivyosema wakati nakabidhiwa cheti cha ushindi na Mwenyekiti wa NEC (Tume ya Taifa ya Uchaguzi), ushindi huu si wa wana CCM peke yao bali ni wa Watanzania wote," alisema.

Alipongeza NEC kwa kusimamia vizuri uchaguzi wa mwaka huu, huku akiwashukuru viongozi wa dini kwa kuongoza vyema dua na sala katika kipindi chote cha uchaguzi na kumaliza salama.



Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, akihutubia wakati wa sherehe ya kuapishwa Rais Dk. John Magufuli, katika Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Museveni atoboa siri ya maendeleo Afrika

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni, amewataka viongozi wa Afrika kusimama katika misingi minne iliyowekwa na wapigania uhuru wa nchi za Afrika, ambayo ni ukombozi wa watu, ustawi, ulinzi wa kimkakati na undugu.

Alisema viongozi wa Afrika wanapaswa kusimama katika misingi hiyo ili kuwashinda aliowaita 'vibaraka wa ukoloni'.

Aliyasema hayo jana katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma wakati wa sherehe za kuapishwa kwa Rais John Magufuli, shehere iliyohudhuriwa na maelfu ya wananchi, viongozi wa kiserikali kutoka ndani na nje ya nchi.

Rais Mauseveni alisema wakati wa ukoloni kulikuwapo na vibaraka wa wakoloni, lakini kulikuwapo na viongozi waliosimama imara kutetea maslahi ya Waafrika, ikiwamo kupigania uhuru mmojawapo ni Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Alisema hata baada ya kupatikana kwa Uhuru kwa nchi za Afrika, vibaraka hao bado wapo, na kwamba njia pekee ya kuwashinda ni kusimama katika misingi hiyo minne.

"Kwanza ni ukombozi, ujio wa viongozi hapa ni juhudi zilizofanywa na Mwalimu Nyerere, pili ni ustawi kwamba lazima tujenge uchumi wa kujitegemea, tujikite katika uzalishaji wa mali," alisema na kuongeza:

"Pia tunapaswa kuimarisha ulinzi katika mipaka yetu pamoja na kudumisha undugu miongoni mwetu."

Kadhalika, Rais Museveni alimpongeza Rais Magufuli kwa ushindi alioupata wa kuchaguliwa kwa mara ya pili kuwa Rais.

**RAIS WA ZIMBABWE**

Rais wa Zimbabwe, Emmason Mnangagwa, alisema: "Sisi tunamuangalia Rais Magufuli kama mtu mazalendo. Tanzania imekuwa Taifa la ukombozi wa nchi nyingi za Afrika, nchi nyingi kutoka kusini mwa Afrika zilikuwa hapa na mlizitunza wakati zinapigania uhuru".

Alisema hata wakati wa njaa nchini Zimbabwe, Rais Magufuli pamoja na Rais Museveni walitoa msaada wa mahindi.

**RAIS COMORO**

Naye, Rais wa Comoro, Azali Athumani, alisema urafiki wa Tanzania na Coromo ni wa miaka mingi na utaendelea kudumu miaka yote.

Alisema Tanzania limekuwa Taifa lenye upendo kwa mataifa mengi barani Afrika wakati wote wa shida na raha.

## Ilivyokuwa kiapo cha JPM

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

MAELFU ya wananchi jana walijitokeza kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, kushuhudia sherehe za kuapishwa kwa Rais John Magufuli, zilizopambwa kwa gwaride na maonyesho ya makomandoo wa Jeshi la Wananchi (JWTZ).

Sherehe hizo zilianza majira ya asubuhi kwa wananchi na viongozi mbalimbali wa kiserikali kutoka ndani na nje ya nchi kuwasili uwanjani kisha kufanyika kwa gwaride la kumuaga na kumkaribisha tena Rais Magufuli katika uongozi.

Rais Magufuli aliwasili uwanjani majira ya saa nne asubuhi na kupigiwa mizinga 21 ya kuagwa na baadaye kupigiwa tena miziga 21 ya ukaribisho.

Baada ya kupigiwa mizinga, Rais Magufuli alikagua vikosi vya majeshi ya ulinzi na usalama vilivyoandaliwa, kisha kwenda kula kiapo cha kuwa Rais majira ya saa 4:11 asubuhi kilichoongozwa na Jaji Mkuu, Profesa Ibrahim Juma.

Wengine waliokuwapo wakishuhudia kiapo hicho ni Spika Job Ndugai, Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi.

Baada ya hapo, Rais Magufuli alikabidhiwa silaha za kijadi ikiwamo mshare na ngao vikiwa na maana ya kulinda na kuitetea Tanzania wakati wote.

Muda mfupi baadaye, Makamu wa Rais, Samia Suluhi Hassan, naye alikwenda kula kiapo kisha kurudi jukwaa kuu.

Vikosi vya ulinzi na usalama vilipita kwa ukakamavu mbele ya Rais John Magufuli, kisha kufuatiwa na kikosi cha makomandoo wa JWTZ ambao walitoa burudani ya aina yake kwa wageni.

Pia kulikuwako na kikundi cha ngoma za utamaduni kutoka visiwani Zanzibar.

Katika sherehe hizo, viongozi mbalimbali wa kiserikali kutokana ndani na nje ya nchi walikuwapo kushuhudia kiapo cha Rais Magufuli.

Waliokwapo ni pamoja na Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, Rais wa visiwa vya Comoro, Azali Athumani na Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa.

Wengine ni Makamu wa Rais wa Botswana, Slumber Tsogwane, Waziri Mkuu wa Burundi, Alain-Guillaume Bunyoni, Pamoja na Waziri wa Masumbiji, Carlis Agostinho do Rosario.

Pia walikuwapo marais wastaafu, Ali Hassan Mwinyi, Jakaya Kikwete, Rais Mstaafu wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi na Rais Mstaafu wa Burundi, Syvester Nyandwi.

Jaji Mkuu Prof. Ibrahim Juma, Mawaziri Wakuu Wastaafu, Edward Lowasa, Frederick Sumaye, Pamoja na Mizengo Pinda pia walihudhuria shughuli hiyo ya kitaifa.

Mbali na viongozi hao, walikuwapo pia Spika mstaafu, Anne Makinda, Jaji Mkuu Mstaafu, Joseph Warioba, Makamu wa Rais Mstaafu, Ghalib Bilali.

Vilevile, walikuwapo mabalozi kutoka nchi za Ubelgiji, Burundi, China, Comoro, Cuba, Denmark, Finland, Ufaransa, Indonesia, Iran, Irand, Italy, Kenya na Marekani.

## HABARI KITAIFA

# Kitendawili Spika, Naibu Spika Bunge kuteguliwa leo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI Kuu ya Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), leo inatarajia kufanya kikao chake jijini Dodoma kwa ajili ya kupitisha jina la atakayegombea nafasi ya Spika wa Bunge la Tanzania na naibu wake.

Kwa mujibu wa Katiba ya CCM kifungu cha 104(h), kamati hiyo ina jukumu la kufikiria na kufanya uteuzi wa mwisho wa wanachama wa CCM walioomba kugombea nafasi ya Spika wa Bunge, Spika Baraza la Wawakilishi, Meya wa Halmashauri ya Jiji na Manispaa.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa juzi, Katibu Mkuu wa chama hicho, Dk. Bashiru Ali, alisema mbali na kutoa uamuzi kuhusu nafasi hizo, kikao hicho pia kitapokea taarifa ya awali ya utekelezaji wa mpango wa CCM wa uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

"Agenda ya pili ni kupitia majina ya wanachama waliomba nafasi ya uspika katika Baraza la Wawakilishi na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na muda umeongezwa kwa uspika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na uwakilishi zoezi limekamilika na vikao vya awali vimefanyika.

"Kamati maalum ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa Zanzibar, imeshaketi na kutoa mapendekezo yatakayojadiliwa katika kikao cha sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa," alisema.

Alisema kwa upande wa Uspika wa Baraza la Wawakilishi, walikuwa wamejitokeza watano akiwamo aliyekuwa Spika Zuberi Ali Maulid.

Kwa mujibu wa Katibu Msaidizi, Mkuu wa Oganizesheni wa CCM Taifa, Solomon Itunda, katika nafasi ya Uspika wa Bunge, wanachama 10 wamejitosa akiwamo aliyekuwa Spika wa Bunge la 11, Job Ndugai na naibu wake, Dk. Tulia Ackson.

Wengine waliojitosa kwenye kinyang'anyiro hicho ni mwanachama wa CCM kutoka Mkoa wa Songwe, Stamina Mdolo, Mwanasheria wa Kujitegemea, Barua Mwakilanga, na David Meshack ambaye aliwahi kutia nia kugombea Jimbo la Kibamba jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo, baadhi ya wanachama waliochukua fomu Ofisi Ndogo ya CCM Dar es Salaam, majina yao bado hayajawekwa wazi huku upande wa Ofisi ya Zanzibar, mwanachama Abdallah Mwinyi akichukua fomu na baadaye kujitoa kugombea nafasi ya uspika.

# Trump sasa maji ya shingo

**WASHINGTON,** MAREKANI

MGOMBEA urais wa Chama cha Democratic, Joe Biden, mbioni kufikia idadi ya kura za kumpeleka Ikulu ya White House, Marekani baada ya kupata kura 253 dhidi ya mpinzani wake, Donald Trump.

Trump ambaye anatetea kiti hicho kupitia Chama cha Republican, hadi jana mchana alikuwa na kura 214, huku akiendelea na kampeni zake za kutaka kusitisha shughuli ya kuhesabiwa kwake katika baadhi ya sehemu za Georgia.

Jimbo hilo ni muhimu katika uchaguzi kwa kuwa bado haijatabiriwa mgombea atakayeibuka mshindi.

Kiongozi huyo kutoka Republican ameahidi kusitisha uhesabu wa kura katika maeneo ambayo anasema kuna udanganyifu unaoendelea.

Kura ambazo zinatakiwa kumpeleka Ikulu yeyote kati ya wagombea hao ni 270 na hadi sasa Biden akizikaribia kuzifikia dhidi ya mpinzani wake.

Ikiwa Trump atapoteza Wisconsin, lazima ashinde Georgia kwa (kura 16), North Carolina (15), Pennsylvania (20) na moja kati ya Arizona (11) au Nevada (6) ili kulinda kiti chake.

Wakati mchakato wa kuhesabu kura ukiendelea nchini humo, kundi la wafuasi wa Republican lilikusanyika jana nje ya Kituo cha kuhesabu kura Kaunti ya Maricopa huko Arizona, wakijibu madai ya mitandao ya kijamii kuwa kura ambazo zinasemekana kuwa za Trump hazitahesabiwa.

Baadhi ya waandamanaji waliingia ndani ya kituo hicho wakisindikizwa na maofisa wa usalama. Asilimia 82 ya kura katika Kaunti ya Maricopa zimehesabiwa huku Biden akiongoza.

Hata hivyo, maofisa walisema wana zaidi ya masanduku 400,000 ya kura ambazo bado hazijahesabiwa.

Kaunti hiyo ambayo inajumuisha eneo la Phoenix, kwa muda mrefu imekuwa ikichukuliwa kuwa ngome ya Republican. Kampeni za Trump zimekosoa mchakato wa kuhesabu kura katika majimbo muhimu ya Wisconsin, Georgia, Pennsylvania na Michigan.

BBC inatabiri kuwa Biden alishinda Michigan na vyombo vya habari vya Marekani vinatabiri kuwa amelinasa Jimbo la Wisconsin, huku matokeo ya Jimbo la Pennsylvania yakiwa bado hayajatangazwa. Kuongoza katika majimbo yote matatu muhimu kunatabiriwa kutampa ushindi Biden.

Biden hajatangaza kuwa ameshinda, lakini alisema kuwa ana uhakika alikuwa njiani kumshinda Trump.

Mamlaka za uchaguzi zilieleza kuwa katika uchaguzi huo uliofanyika Jumanne nchini humo, idadi ya watu waliojitokeza kupiga kura ni kubwa kulinganishwa na katika kipindi cha miaka 120 ikiwa ni sawa na asilimia 66.9.

Biden alikuwa akiungwa mkono na wapigakura milioni 70.5, ikiwa ni idadi kubwa kuwahi kutokea katika historia ya uchaguzi wa Marekani.

Trump alipata kura milioni 67.2, zikiwa ni kura milioni nne zaidi kulinganishwa na alizozipata mwaka 2016.

Juzi, Biden aliwaambia waandishi wa habari huko Wilminton, Delaware kuwa mchakato wa kuhesabu kura ukikamilika, wanaamini watakuwa washindi.

"Nitaongoza kama Rais wa Marekani. Urais siyo taasisi ya washirika wa chama," alisema Biden.

**BBC**


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII

SALAMU ZA PONGEZI



Kamati ya Taifa YA Uongozi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii TASAF, inakupongeza Mhe. **Dkt. Hussein Ali Mwinyi** kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kufuatia ushindi mkubwa ulioupata katika uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 . TASAF inaahidi kuunga mkono dhamira yako ya kuboresha maisha ya wananchi kupitia utekelezaji wa Kipindi cha Pili cha Awamu ya Tatu ya TASAF.

*Pamoja Tuondoe Umaskini*

Mkurugenzi Mtendaji
**Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF**
Barabara ya Jakaya Mrisho Kikwete,S.L.P 2719, Dodoma, TANZANIA,
Simu:**+255 26 2963866**, Nukushi:+255 26 2963871,
Barua pepe: **info@tasaf.go.tz**, Tovuti: **www.tasaf.go.tz**

215975901

# Fundi TANESCO matatani kwa tuhuma za rushwa

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kagera, inakusudia kumfikisha mahakamani mfanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Shamy Magheta.

Mtumishi huyo wa TANESCO anayekabiliwa na tuhuma za kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 500,000 kutoka kwa mwananchi aliyemlaghai kuwa atampelekea huduma ya umeme.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkuu wa TAKUKURU mkoani hapa, John Joseph, alisema mfanyakazi huyo ambaye ni fundi, anadaiwa kufanya tukio hilo kati ya Machi na Aprili, mwaka huu, katika kijiji cha Ruzinga wilayani Karagwe.

"Lakini kwa bahati mbaya eneo hilo ambalo alitaka kupeleka umeme mtuhumiwa, lilikuwa chini ya Wakala Umeme Vijijini (REA) na tayari walikuwa wamekwishaweka ramani kwa ajili ya kusambaza nguzo kupeleka umeme huko," alisema.

Joseph alisema mtuhumiwa huyo kwa kushirikiana na watu wengine, alifanya mbinu ya kuiba nguzo TANESCO na kupeleka katika eneo la mteja huyo na kisha aliichimbia kwa ajili ya kumpelekea umeme.

"Bahati nzuri uongozi wa TANESCO Wilaya ya Karagwe walipata taarifa na kuanza kufuatilia na kubaini kuwa kuna nguzo imepelekwa katika eneo husika isivyo halali na kuagiza nguzo hiyo kung'olewa.

"Baada ya hapo, TAKUKURU tulianza uchunguzi na kubaini kuwa mtuhumiwa alikuwa amejipatia Sh. 500,000 na kupeleka nguzo kinyemela," alisema.

Joseph alisema ufuatiliaji wao ulibaini kuwa fedha hizo hazikufikishwa katika ofisi za TANESCO na kuwa mtuhumiwa atafikishwa mahakamani kwa mashtaka mawili, likiwamo la matumizi mabaya ya ofisi na kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Alitoa wito kwa jamii na watumishi wa umma kuacha kujihusisha na vitendo vya kuomba na kupokea rushwa maana wakibainika watachukuliwa hatua kali za kisheria.



Mjumbe wa Bodi ya Shirika la PharmAccess International, Dk. Fatma Mrisho (katikati), akikabidhi vifaa vya kutolea huduma kwa Mganga Mkuu wa Hospitali ya Mji wa Babati ya Mrara, Dk. Halima Mangiri, kwaajili ya vituo 12 vilivyoko kwenye mradi wa Mamcare unaolenga kuboresha huduma kwa mama wajawazito, mkoani Manyara jana. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Aliyekuwa CHADEMA ajitosa tena Siha

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

ALIYEWAHI kuwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, kati ya mwaka 2015 na 2018 akiwa na kofia ya Chadema, Frank Kisinani, ameomba tena kuchaguliwa kuwania kiti hicho kupitia na Chama cha Mapinduzi (CCM).

Kisinani mwenye nafasi kubwa ya kurejea katika kiti hicho kama atateuliwa na CCM, atachuana vikali na Madiwani wengine ambao ni Dancan Urassa (Karansi), Juma Jani (Sanya Juu) na Humphrey Kifumu (Nasai).

Jana, Katibu wa CCM wa Wilaya ya Siha, Mwanaidi Mbisha, alisema mbali na nafasi hiyo, pia wamo madiwani wanne walioomba nafasi ya Makamu Mwenyekiti.

"Ni kweli mpaka tunafunga shughuli za kupokea fomu za walioomba kuteuliwa na chama, kugombea nafasi ya Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha, ni madiwani wateule wanne pekee wanaotaka uenyekiti na wanne pia wanaotaka umakamu mwenyekiti.

'Kazi iliyopo mbele yetu ni ngumu ya kuchuja majina ya wanaoomba, na kisha sisi kuyapeleka ngazi husika kwa maana ya mkoa. Tutakuja na majina au jina la mtu mwenye sifa stahiki na anayeweza kuisogeza halmashauri kwa mchakamchaka wa maendeleo na sio mtu wa kusukumwa," alisema.

Aidha, walioomba kuchaguliwa kugombea nafasi ya Makamu Mwenyekiti ni pamoja na Susan Kihundwa (Kashashi) ambaye pia ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake wa CCM, Wilayani hapa, Lwite Ndossi maarufu 'Nsonuu' Patrick Kimaro (Ngarenairobi) na Noel Mollel (Ormelili).

Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha, lina historia ndefu ambayo haitasahaulika, kwa kuwa kati ya mwaka 2015 hadi 2018 liliongozwa na madiwani wengi wa CHADEMA, lakini mwaka 2018 lilibadilika na kuongozwa na CCM baada ya madiwani kuihama CHADEMA.

Waliokuwa madiwani wa CHADEMA wakati huo, walikihama chama hicho na kujiunga na CCM, baada ya aliyekuwa Mbunge wa Siha kupitia upinzani, Dk. Godwin Mollel, kujiunga na CCM na kisha kuchaguliwa tena kuwa mbunge kwa tiketi ya chama hicho mwaka 2019.

# Saba wajitosa uenyekiti wa Hai

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WAKATI pazia la uchukuaji na urejeshaji wa fomu za kuomba kuteuliwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kugombea umeya na uenyekiti wa halmashauri likiwa limefungwa rasmi jana, madiwani wateule saba 'wanakesha' Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, kusubiri uamuzi wa chama hicho.

Katibu wa CCM wa Wilaya ya Hai, Kumotola Kumotola, alisema jana kuwa madiwani hao saba, ndio walikuwa wamechukua fomu hadi kufikia Novemba 4, mwaka huu, huku wengine watano wakijitosa kugombea nafasi ya makamu mwenyekiti.

"Mwisho ilikuwa jana Novemba 4, majira ya saa 10:00 jioni. Hivi sasa tunaanza vikao vya kuwajadili wagombea hao kwa ngazi ya wilaya na baadaye tutapeleka mapendekezo yetu mkoani ili kuwapa nao nafasi ya kuanza vikao ngazi ya mkoa," alisema Kumotola.

Wanaotunishiana msuli katika nafasi hiyo na kata zao kwenye mabano ni Edmund Rutaraka (Muungano), Evod Njau (Bomang'ombe) na Martin Munisi (Machame Magharibi).

Wengine waliojitosa kugombea ni John Lengai (Narumu), Jublate Ndossi (Masama Mashariki), Kandaka Kimaro (Masama Kati) na Kehela Kipara (KIA).

Nafasi ya Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, tangu uchaguzi mkuu wa mwaka 2010 hadi 2020, ilikuwa ikishikiliwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Kwa mujibu wa ibara ya 145 na 146 ya Katiba ya Tanzania, Serikali za Mitaa ni vyombo vya haki na vyenye mamlaka ya kushiriki na kushirikisha wananchi katika kupanga na kutekeleza shughuli za maendeleo na utoaji wa huduma katika sehemu zao.

Serikali za Mitaa huanzishwa kwa madhumuni ya kuwahudumia wananchi na kuwapelekea madaraka, kwa kuwajengea uwezo wa kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni.

Kazi za jumla na za lazima za serikali za mitaa, ziko katika Sheria za Serikali za Mitaa Sura 287 na 288, Toleo la 2002. Awali kabla ya mapitio, zilikuwa chini ya Sheria Namba 7 na 8 za Mwaka 1982.

HABARI KITAIFA

# Akutwa na kesi ya kujibu madai kubaka mwanafunzi

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Geita Mkoa wa Geita, imemkuta mkazi wa Bukondo Nestory Nkola (19), kuwa ana kesi ya kujibu baada ya upande wa mashtaka kufunga ushahidi wake.

Uamuzi huo mdogo ulitolewa na Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Sosthenes Kiiza, baada ya upande wa mashtaka kufunga ushahidi.

Kiiza alisema mshtakiwa huyo anakabiliwa na kosa moja la kubaka msichana mwenye umri wa miaka 16 ambaye ni mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Mapinduzi.

Alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, James Pallangyo, alipeleka mahakamani mashahidi wanne na vielelezo vitatu.

Hakimu Kiiza alisema mwathirika wa tukio hilo, alithibitisha mahakamani kuwa mshtakiwa ni mpenzi wake na kudai kuwa baba wa binti huyo aliwakuta mshtakiwa na binti yake wakiwa ndani wakifanya mapenzi, na kwamba baada ya tukio hilo baba wa binti huyo alitoa taarifa kituo cha polisi na mshtakiwa huyo akakamatwa.

Alisema upande wa mashtaka umethibitisha kosa hilo na mahakama imemwona mshtakiwa ana kesi ya kujibu. Mshtakiwa huyo alidai mahakamani kuwa atajitetea kwa kiapo hana shahidi.

Hakimu Kiiza aliahirisha kesi hiyo hadi Novemba 25, mwaka huu kwa ajili ya mshtakiwa huyo kutoa utetezi wake.

Aidha, alisema mshtakiwa ataendelea na dhamana yake hadi tarehe iliyopangwa kwa ajili ya kutoa utetezi wake.

Awali akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali, James Pallangyo, alidai kuwa tarehe isiyofahamika kati ya Januari na Machi 8, mwaka huu katika Kijiji cha Bukondo Mkoa wa Geita, mshtakiwa alimbaka msichana mwenye umri wa miaka 16 ambaye ni mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Mapinduzi.

# Mawasiliano ya barabara sasa yarejeshwa Mtwara

**Na Thereza Chimagu**

WAKALA wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) umefanikiwa kufanya ukarabati wa barabara iliyoharibiwa na mvua na kusababisha kukatika kwa mawasiliano kati ya Vijiji vya Libobe na Ming'wena vilivyopo Kata ya Libobe katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara mkoani humo.

Akizungumzia ujenzi wa barabara hiyo, Meneja wa TARURA Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, Mhandisi Patrick Kanyagha, alisema baada ya kupata changamoto ya kukatika kwa barabara hiyo waliomba fedha za dharura kutoka TARURA Makao Makuu na kupatiwa shilingi milioni 185 ambazo zilitumika kutengeneza barabara iliyopo kati ya Kijiji cha Libobe hadi Ming'wena yenye urefu wa Kilomita 4.8, kwa kiwango cha changarawe ili wananchi waendelee na shughuli zao za kiuchumi.

"Kipande hiki ni sehemu ya barabara ya Libobe - Ming'wena - Likwidi - Mtama yenye jumla ya urefu wa Km 19, na tulichukua maamuzi ya kutengeneza baada ya mvua kuharibu miundombinu ya barabara pamoja na kuathiri makazi ya wananchi, ili kurejesha mawasiliano na kuwezesha wananchi kusafirisha bidhaa zao kama hapo awali," alisema Mhandisi Kanyagha.

Meneja huyo alisema baada ya kupatiwa fedha hizo, kazi walizozipa kipaumbele zilikuwa ni kurejesha tuta, kujenga "box culvert" mpya ambapo zimejengwa nene, kujenga mtaro wa maji ya mvua na kurejesha tabaka la changarawe urefu wa kilomita 3.5, ambapo kazi zote zimekamilika na mawasiliano yamerejea katika vijiji hivyo.

Naye, Majid Rashid, mkazi wa Kijiji cha Ming'wena, alipongeza serikali kwa kutengeneza barabara katika eneo hilo kwani imesaidia kupunguza kero ya usafiri na kufanya wananchi waendelee na shughuli zao kama hapo awali.

"Tunaishukuru TARURA kwa kutujali na kutufanyia ukarabati wa haraka kwani tulikuwa na changamoto ya usafiri kutoka hapa hadi kufika barabara kuu ya Mpapora kwani magari na hata pikipiki yalikuwa hayapiti kabisa, lakini baada ya matengenezo ya barabara tumefaidika sana na imerahisisha mawasiliano," alisema Rashid.

Naye Somoe Kankunje, mkazi wa Kijiji cha Ming'wena, alisema upatikanaji wa huduma mbalimbali za kijamii katika eneo hilo umerahisishwa na ukarabati wa barabara hiyo kwani hawapati shida ya usafiri na wanaendelea na biashara zao kama awali bila matatizo.

TARURA katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara inaendelea na kazi mbalimbali, zikiwamo za matengenezo ya barabara na vivuko katika wilaya hiyo, ili kuwawezesha wananchi kusafiri na kusafirisha mazao pamoja na bidhaa zao kwa urahisi.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Vyama vya siasa vipatiwe ruzuku kwa kukidhi vigezo

**BAADHI** ya vyama vya siasa nchini, vimekuwa vikilalamikia kutokupewa ruzuku ya serikali, huku vikidai kuwa hali hiyo inavifanya kupata vikwazo katika kutekeleza majukumu yao.

Malalamiko hayo yamekuwapo kwa muda mrefu tangu baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu wa mwaka 1995.

Serikali kwa dhamira njema, mwaka 1995 ilitoa ruzuku kwa vyama vyote vya siasa vilivyokuwa na usajili wa kudumu, lengo likiwa ni kuviwezesha kushiriki uchaguzi huo.

Hata hivyo, itakumbukwa kuwa baada ya uchaguzi huo, kuna matukio yaliyoifanya serikali kuweka utaratibu rasmi wa utoaji wa ruzuku hiyo, hivyo vyama vingi vikajikuta vikikosa fursa hiyo.Miongoni mwa matukio yaliyoifanya serikali iweke utaratibu wa kisheria wa utoaji wa ruzuku hiyo, ni matumizi mabaya ya fedha hizo pamoja na migogoro iliyoibuka kwenye vyama ya kugombania fedha hizo.

Kwa mujibu wa utaratibu huo, vyama vilitakiwa kupata ushindi wa angalau asilimia 5 ya kura zote pamoja na kuwa na wawakilishi bungeni.

Kuanzia uchaguzi mkuu wa mwaka 2000, vyama vichache ambavyo vimekuwa vikinapata matokeo mazuri kwenye uchaguzi vilianza kupata ruzuku.

Kwa mfano kabla ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu vyama vilivyokuwa vinapata ruzuku ni CCM, CHADEMA, CUF, ACT-Wazalendo na NCCR-Mageuzi.

Hata hivyo, vyama vingine vimekuwa vikilalamikia kutopata ruzuku, hivyo kuishinikiza serikali ivipatie kwa madai ya kutekeleza majukumu yao.

Jumapili katika hafla ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kumkabidhi cheti cha ushindi Rais John Magufuli jijini Dodoma, vyama hivyo vilirudia kukumbushia umuhimu wa kupatiwa ruzuku.

Vyama hivyo visivyo na uwakilishi bungeni vilimuomba Rais Magufuli kuviwezesha ruzuku ili kusaidia shughuli za kiutendaji ndani ya vyama vyao.

Akizungumza kwa niaba ya wagombea 10 wa urais ambao walishiriki kwenye uchaguzi mkuu mwaka huu, mgombea wa Chama cha ADC, Queen Sendiga, alisema vyama hivyo vinaomba uwezeshaji ruzuku japo kwa asilimia kidogo ili kusaidia kufanya shughuli za kiutendaji ndani ya chama.

Walimuomba avifikirie vyama hivyo na kama inawezekana vipatiwe chochote ili vifikie malengo ya kuwafikia Watanzania kipindi hiki.

Pamoja na umuhimu wa ruzuku kwa vyama vya siasa, hatuoni sababu za kuvipa ruzuku fedha za walipakodi nje ya utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa sheria.


Utaratibu uliopo ni mzuri kwa sababu unavifanya vyama kuwa makini na kuwajibika kufanya shughuli za kisiasa; kwa maana ya kwenda kwa wananchi na kuwashawishi wavikubali kisha kuvipa kura wakati wa uchaguzi kama vyama vingine vilivyofanya na kufanikiwa.

Aidha, vyama makini vya siasa vinaweza kupata fedha zake bila kutegemea ruzuku kwa kuuza kadi, kofia, sare, bendera, vipeperushi, michango ya wanachama, harambee na kuchangiwa na marafiki pamoja na wadau.

Ushauri wetu kwa serikali ni kuwa isikubali kutoa ruzuku kwa vyama visivyo na uwakilishi, kwa kuwa nchi ina mahitaji ya huduma muhimu kwa wananchi pamoja na miradi mikubwa inayohitaji fedha nyingi.

Vyama visivyo na uwakilishi vijipange kujenga mtandao wa wananchama, wadau pamoja na kuweka mikakati ya kusaka fedha kupitia njia tulizozitaja.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Maagizo haya yakitekelezwa basi ni ukombozi wa Machinga

Na Sabato Kasika

**LEO** ni zaidi ya miaka miwili tangu wakuu wa wilaya nchini waagizwe kusimamia halmashauri zao za utawala, ili zitenge maeneo maalum kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo, maarufu kama Wamachinga.

Aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMi), Selemani Jafo, aliagiza akifungua Mkutano Mkuu wa Shirika la Umoja wa Wamachinga Tanzania (SHIUMA).

Mkutano huo ulifanyika Dodoma, huku akisema Wamachinga ni watu muhimu katika kukuza uchumi wa Tanzania, akiweka wazi kuwa wafanyabiashara wadogo ndio wanaoleta muunganiko wa watu katika kada mbalimbali.

Anawataja watu hao kuwa ni pamoja na wasomi wenye shahada, astashaada, kidato cha sita, kidato cha nne, darasa la saba na wasiosoma kabisa, kwamba wote wanaunganika na kufanya biashara kama Wamachinga.

Kwa mujibu wa Jafo, wakuu wa wilaya wana wajibu wa kuratibu na kuhakikisha kuwa wanatenga maeneo ya wamachinga ili wafanye bishara zao kwa utaratibu bila kuvunja sheria za nchi.

Anasema, kati ya Watanzania zaidi ya milioni 50, walioajiriwa serikalini na sekta ya umma ni 520,000 na kwamba kundi kubwa ni la watu ambao ama wamejiajiri au wameajiriwa katika sekta binafsi.

Jafo anasema, kundi kubwa ni wale watu wanaojishughulisha kwa kutafuta riziki zao wenyewe ambao watu hao ndio asilimia kubwa wako katika kundi la wamachinga, na kwamba kuna umuhimu wa kuwatengea maeneo.

Muungwana anaungana na Jafo kwamba, wakuu wa wilaya wawatengee Wamachinga maeneo ya biashara, kwa kuwa wengi wao wamekuwa wakifanyia shughuli zao hata kwenye maeneo hatarishi.

Miongoni mwa maeneo hatarishi ni chini ya nyaya kubwa za umeme, lakini baadhi ya Wamachinga hufanyia shughuli zao huko kana kwamba, wako salama na kumbe wanaweza kujikuta katika hatari.

Si huko tu bali wengi wa Wamachinga kwa sasa, hupanga biashara kandokando ya barabara, hali ambayo inaweza kusababisha wakakumbana na ajali zitokanzo na vyombo vya moto, yakiwamo magari.

Ni vyema maagizo yaliyotolewa na Jafo yatekelezwe, kuwa haipendezi kuona wamachinga kuwa katika mazingira ambayo yanawafanya kila wakati kutokuwa na uhakika wa usalama wao na hata wa kipato cha kila siku.

Zipo halmashauri ambazo zimeanza kutekeleza maagizo hayo ikiwamo ya Ub Ubungo Dar es Salaam inayojenga masoko mawili, kwa ajili ya wamachinga wa Mbezi Mwisho, ambayo hata hivyo, inaelezwa kuwa hayatoshi.

Masoko hayo yanajengwa pembeni mwa stendi mpya ya mabasi ya mikoani na lingine kando ya barabara ya kuelekea Goba, lakini Wamachinga wameanza kulalamika kuwa hayatoshi, ingawa hawajahamia huko.

Mhandisi mmojawapo anayesimamia ujenzi wa soko lililo pembeni mwa stendi ya mabasi ya mikoani, alishawahi kusema lina uwezo wa kuchukua Wamachinga 700 litakapokamilika.

Lakini inaelezwa na viongozi wa Wamachinga wa Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam, kuwa wafanyabiashara hao wapo zaidi ya 1000, hivyo soko hilo na ililopo kando ya barabara ya Goba, bado hazitakidhi kuwachukua wote.

Kama kweli ndivyo ilivyo, basi zinahitajika jitihada za makusudi, kutengwe maeneo ya kutosha kwa ajili ya kundi hilo, liweze kufanya biashara kwa uhakika ili lijikwamue kiuchumi.

Ninatambua kwamba, serikali imejiwekea mkakati wa kutengeneza masoko mazuri na ya kisasa kwa kuweka mazingira bora kwa wamachinga kufanya biashara zao katika maeneo stahiki, kinachotakiwa sasa ni utekelezaji.

Lakini pia ni vyema soko lolote linalojengwa, wafanyabiashara wadogo waliokuwapo awali katika eneo husika wajulikane na kupewa kipaumbele kwa kugawiwa maeneo ya kufanya biashara mara majengo yanapokamilika.

Hatua hiyo inasaidia kuepusha ama kuwapo mchezo wa kuuzia wengine wanaotoka maeneo ya mbali na kusababisha wenyeji kukosa, na hivyo kuwafanya waendelee kuwa katika maeneo hatarishi.

Jambo zaidi la kuzingatia katika ujenzi wa masoko ni kuwapo miundombinu yote kuanzia maji, vyoo, barabara, usafiri na mengine mingi ambayo huwa inasababisha wamachinga wasihamie katika masoko mapya.

TANGAZO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
**SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA**
**TASAC**

# Salamu za Pongezi



**Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli**



**Mhe. Samia Suluhu Hassan**

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa **SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA (TASAC)** inatoa pongezi kwa Rais Mteule **Dkt. John Pombe Magufuli na Makamu wa Rais Mteule Samia Suluhu Hassan kwa ushindi katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2020.**

Ushindi mkubwa walioupata ni tafsiri tosha kuwa Watanzania wana imani na viongozi wao kutokana na uwajibikaji, uadilifu na uzalendo waliouonesha kwa Taifa katika miaka mitano ya kwanza.

Jengo la PPF Tower, Sakafu ya 7 na 8, Kiwanja Na. 20/21, Mtaa wa Garden/Ohio,
S. L. P. 989, Dar es Salaam - Tanzania, Simu: +255 222 127 314, Nukushi: +255 222 127 313,
Barua Pepe: dg@tasac.go.tz, info@tasac.go.tz, Tovuti: www.tasac.go.tz

# RC Morogoro: Uchaguzi umekwisha, tuchape kazi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare (pichani), amesema uchaguzi umekwishwa, hivyo wananchi watoe ushirikiano kwa viongozi waliochaguliwa ili kuwasaidia kutimiza ahadi za kuwaletea maendeleo walizotoa wakati wa kampeni.

Sanare alitoa agizo hilo wakati akizungumza na waandishi wa habari, akiwashauri Watanzania kukubaliana na matokeo ili wananchi waendelee na shughuli za kujiletea maendeleo.

Aliwashauri kutojihusisha na maandamano yenye lengo la kupinga matokeo ya yaliyotangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Alisema Kamati ya Ulinzi na Usalama ya mkoa huo ipo kwa ajili ya kulinda amani ya Watanzania , hivyo haitosita kuchukua hatua za kisheria kwa yeyote au kikundi chochote kitakachojihusisha kwenye maandamano ya kupinga matokeo ya uchaguzi.

"Kuna kikindi cha watu wanasema watafanya maandamano endelevu ya kupinga matokeo ya uchaguzi, na wamepanga kufanya hivyo siku yoyote... nataka niwaambie Tanzania nzima ulinzi na usalama ni endelevu," alisema Sanare.



Alisema kwa kuwa uchaguzi umekwisha, wananchi natakiwa kuchapa kazi ili kujiletea maendeleo.

Aliwashukuru wananchi wa mkoa huo kwa kutoa ushirikiano katika kipindi chote cha kampeni na uchaguzi kwa kuwa wasikivu, kufuata maelekezo kwa kudumisha amani wakati wote.

# Siri kuboreka maisha ya wananchi yatajwa

**Na Mwandishi Wetu**, SINGIDA

MABADILIKO ya maisha ya wananchi na uchumi wa Mkoa wa Singida yameelezwa kuwa hayatokani na kilimo cha alizeti pekee, bali yamechangiwa na kilimo cha mazao mengine pamoja na shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Watafiti ambao walifanya utafiti Mkoa wa Singida hivi karibuni, wamebaini ukweli wa nini kilichoufanya mkoa kupaa kiuchumi baada ya kuwapo kwa dhana ya wananchi kwamba kilimo cha alizeti ndicho kimeupaisha mkoa huo kimaendeleo.

Mtafiti wa Mradi wa Utafiti wa Sera za Kilimo Barani Afrika (APRA), Dk. Christopher Magomba, alisema hayo wakati akiwasilisha mada ya utafitihuo hivi mjini Morogoro kwa waandishi wa habari wakati wa kikao kazi cha kutoa matokeo yake kilichokuwa kimeandaliwa mradi wa APRA.

Dk. Magomba alisema kuwa utafiti wa zao hilo ulifanyika kuanzia Julai 2018 katika vijiji 15 kutoka wilaya mbili za Iramba na Mkalama. Alisema kilimo cha mazao mengine na shughuli zingine za kiuchumi, vyanzo mbadala na miradi midogo midogo inayofanywa na kaya nayo imechangia kuinua uchumi wa mkoa huo.

Alitolea mfano kilimo cha mahindi ambacho ni asilimia 83.86, ni moja ya zao ambalo linaonyesha kuchangia maendeleo mkoani humo ukilinganisha na alizeti ambalo katika utafiti wao walioufanya katika Wilaya ya Iramba na Mkalama lilionyesha kuwa na asilimia 71 tu. Dk. Magomba alitaja mazao mengine ambayo yameonyesha kufanya vizuri na kuongeza kipato katika mkoa huo kuwa ni vitunguu, nyanya, mtama na pamba.

Naye Mtafiti Mwandamizi masuala ya kilimo na jinsia, Dk. Devotha Kilave, alisema kuwa ushiriki wa wanawake katika kilimo biashara umetoa mchango mkubwa katika kuwawezesha kukidhi mahitaji yao ikiwamo na kushiriki kwenye mambo mbalimbali ya kutoa maamuzi ndani na n je ya kaya zao.

Dk. Kilave alisema ili wanawake waweze kuendelea vizuri katika hali halisi ya maisha ya kila siku, kilimo biashara kwao kina mchango mkubwa kuwawezesha kujikwamua katika umaskini na utegemezi.







# MATANGAZO

Lodhia group of companies

## NAFASI ZA KAZI KATIKA KIWANDA KIKUBWA CHA CHUMA NA PLASTIKI

Kiwanda cha Lodhia cha Chuma na Plastiki, kilichopo kisemvule Mkuranga kinakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa katika nafasi zifuatazo. Hii ni fursa ya kipekee kwa Vijana wenye ndoto ya kufanya kazi na kupata ujuzi sahihi wa uendeshaji mitambo ya kisasa katika viwanda vya chuma.

**MHANDISI UMEME NA MITAMBO (WALIOHITIMU MWAKA HUU)-NAFASI NNE**
- Wahitimu wa uhandisi wenye shahada ya kwanza na kuendelea
- Ufaulu mzuri wa masomo ya uhandisi
- Awe na ujuzi imara katika Umeme, Mawasiliano na PLC
- Uwezo wa hali ya juu wa mawasiliano.
- Sharti awe tayari kufanya kazi zamu ya usiku na mchana

**MHANDISI WA UMEME NA MITAMBO (AWE NA UZOEFU)-NAFASI TATU**
- Wahitimu wa uhandisi wa Umeme wenye kiwango cha chini cha shahada ya kwanza
- Ufaulu mzuri wa masomo ya uhandisi
- Uzoefu wa miaka 3 mpaka 5 kazini.
- Uzoefu wa moja kwa moja katika shughuli za uzalishaji kwenye viwanda vikubwa. (Uzoefu katika viwanda vya chuma ni faida kwa muombaji)
- Sharti awe na utayari wa kufanya kazi zamu ya mchana au usiku
- Uzoefu katika vifaa vya umeme vya kisasa, Mawasiliano na PLC

**MHANDISI WA UMEME (AWE NA UZOEFU)-NAFASI TATU**
- Wahitimu wa uhandisi umeme wenye ya shahada ya kwanza na kuendelea
- Ufaulu mzuri wa masomo ya uhandisi
- Uzoefu zaidi ya miaka 5 katika kazi za Umeme mkubwa, uwekaji transifoma, VCB, njia za kusambaza Umeme na kadhalika.
- Uwezo wa kuweka kebo na HT, Laini za umeme za LT, Usambazaji wa Umeme kutoka kwenye transifoma kwenda kwenye kitua cha usambazaji kiwandani.
- Ujuzi wa kutengeneza mitambo ya DC na AC
- Uwezo wa Kuweka makadirio ya kebo za Umeme za kiwandani
- Uzoefu wa kufanyia kazi umeme wa viwandani. (Ikiwa ni viwanda vya chuma ni bora kwa muombaji)
- Sharti awe tayari kufanya kazi zamu ya usiku na mchana

**MHANDISI MITAMBO (WALIOHITIMU MWAKA HUU)-NAFASI NNE**
- Wahitimu wa uhandisi mitambo awe na shahada ya kwanza ya uhandisi na kuendelea
- Awe na msingi mzuri wa kielimu
- Ujuzi wa mitambo maji maji, Nyumatiki, Ubadilishaji gia,Gia boksi, beringi na kadhalika
- Sharti awe tayari kufanya kazi zamu ya mchana na usiku

**MHANDISI MITAMBO MPANGILIO NA UENDESHAJI-NAFASI TATU (UZOEFU WA UENDESHAJI MITAMBO YA CNC)**
- Awe na stashahada ya uhandisi mitambo
- Awe na msingi mzuri kielimu
- Uzoefu wa miaka 2-3 (Katika viwanda vya chuma)
- Awe na uwezo wa kupangilia kituo mbadilisho cha CNC
- Awe na uwezo wa kuendesha mashine za CNC zinazotumika viwanda vya chuma.
- Sharti awe tayari kufanya kazi kwa zamu mchana na usiku.

**MHANDISI MITAMBO (WAHANDISI MZOEFU DARAJA LA JUU)-NAFASI MBILI**
- Mhitimu uhandisi mwenye shahada ya kwanza au Zaidi
- Awe na msingi mzuri kielimu
- Uzoefu wa zaidi ya miaka mitano (5) kwenye kiwanda chochote kikubwa cha uzalishaji (Viwanda vya chuma ni bora zaidi)
- Uzoefu wa kadi ya kiotomatiki. Lazima awe na ujuzi mzuri katika ubunifu na uwezo wa kuelewa michoro ya kiuhandisi.
- Lazima awe na uwezo wa kubuni michoro ya sehemu/shughuli yoyote ya kiuhandisi mitambo.
- Ujuzi wa mitambo maji maji, Nyumatiki, Ubadilishaji gia , Gia boksi, beringi na kadhalika
- Lazima awe na Uzoefu wa kiutendaji kwa vitendo.
- Sharti awe tayari kufanya kazi kwa zamu mchana na usiku

**SIFA ZA JUMLA KWA WOTE:**
- Muombaji awe Mtanzania
- Muda wa mafunzo kwa vitendo hautahesabika kama Uzoefu
- Muaminifu
- Mchapa kazi
- Anayefundishika haraka
- Mtizamo chanya wa mambo

**NAMNA YA KUTUMA MAOMBI:**
Tuma CV, barua ya nafasi unayomba, vyeti vyako vya Elimu kwa anuani ya barua pepe ifuatayo. **info-dar@lodhiagroup.co.tz**

**Au**
**Tuma CV, Barua ya nafasi unayoomba, vyeti vyako kwa anuani ya Lodhia Steel Industries Ltd S.L.P 75778, Dar es Salaam-Tanzania.**

**ZINGATIA:**
Ukitumia barua pepe usitume tena kwa sanduku la posta. Endapo utatuma kwa barua pepe na Sanduku la barua maombi yako hayatashulikiwa.

**MUHIMU:**
Kichwa cha habari cha barua pepe kisomeke nafasi unayomba kwa usahihi bila kukosea Mfano. MHANDISI UMEME NA MITAMBO (WALIOHITIMU MWAKA HUU).

**MWISHO WA KUTUMA:**
Tutapokea maombi ya kazi mwisho tarehe **15/11/2020.**

**ZINGATIA:**
Tutawasiliana na waombaji watakaotimiza vigezo vya nafasi anayoomba na watakaofuata maelekezo ya kuomba nafasi husika kwa usahihi. Hii ni sifa kuu ya kwanza kufuata maelekezo kwa usahihi.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS,**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM**

# TANGAZO

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam anawatangazia wananchi wote kujiandaa kutumia kituo kipya cha mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani kwa huduma za usafiri, usafirishaji.shughuli za biashara, uwekezaji na Uchumi katika kituo kipya cha mabasi cha Mbezi Luis kuanzia tarehe 30 Novemba, 2020 badala ya kutumia kituo cha mabasi cha Ubungo kinachotumika hivi sasa.

Pia, anawatangazia wananchi wote kuomba kufanya shughuli mbalimbali zinazojumuisha:-

- » Maeneo ya Ofisi za kukatia Tiketi.
- » Maeneo ya kutolea huduma za benki, kampuni za Simu, uwakala na wakala wa Fedha.
- » Maduka ya Jumla, Supermarket na Mini Super market.
- » Zahanati, Maabara na Famasi
- » Cafe & Fast Food, Migahawa,Vinywaji na baa.
- » Mae!'! 0 ya Wafanyabiashara wadogo na wa Kati,.
- » Sehemu ya kuhifadhia mizigo
- » Sehemu ya kuweka Ofisi.
- » Sehemu ya mazoezi (Gym)
- » Vending Mashine / ATM
- » Maeneo ya Maduka ya bidhaa kama vile Vipuri, vifaa vya kieletroniki, vifaa vya Michezo, vitam baa, Nguo, Magodoro, Vito, Vipodozi, Mapambo, Saloon, Urembo, viatu, nguo za watoto z wanawake na wanaume, pembejeo za Kilimo na Mifugo, Samani (Furniture), Stationary, kioski, Carpets/ pillow / curtains

>- Maombi ya upangishaji wa maeneo / Sehemu zilizotajwa yatumwe kuanzia tarehe 09 Novemba, 2020 hadi tarehe 25 Novemba,2020 kwa njia ya mtandao kwa kutumia anuani www.pangisha.tamisemi.go.tz.

Wamachinga, Baba na Mama Lishe wanapaswa kuandika barua ya maombi ya kufanya shughuli zao kwenye maeneo waliyotengewa na kuwasilisha utambulisho kutoka kwa Mtendaji wa Serikali ya Mtaa anapoishi muornbaji.

Limetolewa na;

**Sipora J. Liana**
**MKURUGENZI WA JIJI**

Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Jiji, Ukumbi wa Jiji, 1 Barabara ya Morogoro, S. L.P: 9084, 11882 Dar es Salaam,
Unaweza pia kuwasiliana nasi kwa Simu: +255212355115, Nukushi: 0222125589, Barua pepe - cd@dcc.qo.tz

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO



# Salamu Za Pongezi

## Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli & Mhe. Samia Suluhu Hassan

Uongozi, Menejimenti na Watumishi wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi) tunaungana na Watanzania wote kukupongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitano kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 28 Oktoba, 2020.

Tunaahidi kuendelea kuimarisha miundombinu inayosimamiwa na Sekta ya Ujenzi ambayo ni kichocheo cha maendeleo ya kiuchumi kwa wananchi ambao wamekuchagua kwa kishindo.


***"Tuienzi, Tuilinde na Kuitunza Miundombinu Yetu kwa Maendeleo ya Sasa na ya Vizazi Vijavyo"***








@wizaraUUM www.mwtc.go.tz wizarauum




Ukurasa 13

TANESCO na ujenzi wa nyumba zetu

BUFE

IJUMAA NOVEMBA 6, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 12

Hekaheka ya tabianchi ilivyokaribisha dhiki kwa wanakijiji wavuvi Mkuranga

UCHUMI

# Mradi maji unaoibua uchumi wa kuzalisha vitunguu Babati

**Na Renatha Msungu, aliyekuwa Babati**

MATUNDA ya kuwatumia wataalamu wa ndani wa Wizara ya Maji, kutekeleza miradi ya maji kwa utaratibu unaoitwa 'force account' umeleta matokeo chanya kwa wananchi, kupata huduma ya maji yanayojitosheleza.

Kimsingi 'force account' ni akaunti maalum inayotumika kuhudumia mahitaji ya dharura, hasa kwenye halmashauri ambayo imewasaidia wakulima wa Manyara kwa kiasi kikubwa kuendesha kilimo na biashara ya vitunguu.

Hivi sasa idadi ya wananchi wanaopata maji katika mradi unaoitwa Arri Harsha, ni zaidi ya 5000 na mradi utakapokamilika, utahudumia wananchi 32,000 na utakuwa na vituo vya kuchotea maji 55.

Hadi sasa vituo 14 vimeshakamilika vikitoa huduma ya maji bila matatizo, hali inayowahamasisha wakazi wa eneo hilo kulima vitunguu kuwaongezea kipato, utekelezaji wake ni mkubwa, ukiwalenga wananchi wa mitaa ya mji mdogo wa Dongobesh, ukiwa na thamani ya Sh. bilioni 1.6.

Mradi huo unatarajiwa kuwawawezesha wananchi wa vijiji vyote saba kupata majisafi na salama na inayotosheleza karibu na makazi yao, umbali usiozidi mita 400.

Ni hatua inayotajwa kuwawezesha wananchi kutekeleza shughuli za uingizaji kipato, ikiwamo kilimo, ambapo zao la vitunguu ni maarufu katika eneo hili.

Wizara ya Maji hivi sasa inatekeleza baadhi ya miradi ya maji nchini, kwa kutumia utaratibu 'force account' lengo ni kuharakisha na kupunguza gharama za utekelezaji wa miradi ya maji na kufikia malengo ya kitaifa katika sekta ya maji kwa muda uliopangwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Babati (BAWASA), Mhandisi Iddy Msuya, anasema hadi hadi mwezi Agosti, 2020 kwa kutumia 'force account' serikali imefanikisha miradi ya maji 668, inayohudumia jumla ya wananchi wapatao 4,328,254 na kutumia Sh. 203,196,609,301.55.



Ujenzi wa mitambo ya kuchuja Maji Mutuka wilayani Babati. **PICHA: RENATHA MSUNGU.**

Anasema, mkoa Manyara katika maeneo mengi, kuna miradi inayotekelezwa kwa utaratibu huo, imeshakamilika mapema na kuanza kutoa huduma, akitaja baadhi ya wanaofurahia matunda ni wakazi wa Wilaya ya Mbulu katika Kata za Bashay na Yaeda Ampa.

Pia, kunatajwa maeneo mengine ni Arri Harsha, ambako hivi sasa wananchi wanapata huduma ya majisafi, salama na inayojitosheleza baada ya mradi kukamilika na kuanza kutolewa huduma ya maji katika vituo 14.

**BOSI BAWASA**

Mkurugenzi Mtendaji wa BAWASA, Mhandisi Iddy Msuya, anaiambia Nipashe kuwa vijiji vilivyopo katika eneo la mradi na imeshakamilika ni Arri, Hyseng Yaeda Ampa Mangisa, pia kuna ambavyo havijakamilika; Yaeda Kati, Harsha, Bashay na Hyseng

Anasema, suala la kupata majisafi na salama kwa baadhi ya maeneo ilichukua muda, kutokana na utekelezaji wake ulisuasua, sababu ni makandarasi kutozingatia mikataba, pia gharama kubwa zilizojitokeza katika utekelezaji.

Msuya anasena miradi iliyopo, ilianza kwa mkandarasi wa kwanza aliyeishia ngazi ya asilimia 20 pekee na kukosekana ufanisi huo, serikali iliamua kutekeleza sehemu iliyobaki kwa kutumia wataalamu wake.

Anasema, awali kabla ya mradi kuanza kutoa huduma wananchi walipata shida katika jukumu la kupata maji, kwa kutumia maji yasiyo salama katika vyanzo visivyo na uhakika.

Pia, Mkurugenzi huyo wa BAWASA, anasema awali maji yalitumika pia kunufaisha mifugo, hivyo yalisababisha magonjwa ya kila mara yanayosababishwa na matumizi ya maji yasiyo safi na salama, sasa kukamilika kwake kunawaingiza wananchi katika afya ya maji

"Kwa haya maji ya bomba ya mradi huu, sisi BAWASA na wananchi tumefurahi sana kwani afya zetu ni salama kabisa, hakuna magonjwa," anafafanua Mhandisi Msuya.

**WAKAZI BABATI**

Mkazi wa eneo la Babati, Thomas Bayo, anasema kutokana na wananchi wa Kata za Bashay na Yaeda Ampa kupata adha ya maji kwa muda mrefu, sasa wanapata maji ya uhakika, upo umuhimu kwa wananchi katika eneo hilo kutunza miundombinu na vyanzo vya maji ili miradi iwe endelevu.

"Tunaishukuru serikali kwa maendeleo haya, kwa kuleta huduma hii ya maji karibu, kinamama wanachota maji bombani bila shida," anasema Bayo.

Hadi sasa, wakazi wa maeneo hayo wanaendesha kilimo cha vitunguu ambacho uwaingizia kipato chao cha kila siku.

Mkazi Emmanuel Hawaq, anasema mradi wa maji umesaidia kubadilisha maisha ya wakazi wa maeneo haya kutokana na kuwa wengi wao hivi sasa wanaendesha kilimo cha mazao ambalimbali.

UCHUMI

# Hekaheka ya tabianchi lilivyokaribisha dhiki kwa wanakijiji wavuvi Mkuranga

## • Wabaki njia panda kilio ‘tufanye nini’
## • Kilimo hakiwalipi, kibarua nacho tabu!

**Na Beatrice Philemon, aliyekuwa Mkuranga**

NI umbali kilomita 95 ulipo mji Mkuranga, mkoa wa Pwani kunapatikana kijiji cha Mdimni katika kata ya Magawa, ambako Alhamisi wiki iliyopita, gazeti hili lilikuwa na simulizi ya ardhi ya kijiji kuliwa na mmomonyoko kutoka baharini.

Tafsiri hiyo ndiyo imekihamisha kijiji, sasa ina makali ya dhiki kwa wanakijiji na kwa namna ya pekee jumuiya ya wavuvi ambayo msamiati kulala njaa ni kawaida kwao, huku wako walioweka kando taaluma hiyo.

Nipashe iliyotua mahali hapo hivi karibuni, iliwashuhudia baadhi ya wanakijiji wavuvi wengi wamekata tamaa ya maisha na imekuwa duni sana, hata kuwapo wenye mitihani ya ‘ntakula vipi’ halo ambayo hakuwa nayo miaka iliyopita.

Mabadiliko ya tabianchi, kwanza yamebadili kina cha bahari, ikiwa imejaa matope, upepo mkali na baharini samaki wamepungua.

Akizungumza kwa niaba ya wavuvi wenzake nje ya nyumba yake akiwa na uso wa huzuni, Omar Kilumbi anasema uvuvi uliwasaidia sana kiuchumi zamani, sasa imekuwa simulizi tofauti.

“Mambo yamekuwa tofauti na nilivyotegemea, mabadiliko ya tabianchi yameathiri shughuli zetu za uvuvi. Hivi sasa fedha ninayopata kutokana na kuuza samaki ni ndogo sana.

“Haiwezi kutosheleza mahitaji ya familia yangu, kwa sababu hakuna biashara ya samaki inayofanyika na bado naendelea kutumia mtumbwi wa asili, ambao hauwezi kwenda kwenye maji mengi au kina kirefu kuvua samaki,” anasema

Kilumbi anasema, awali alikuwa analima, lakini baadaye alikiona kilimo hakifai, akiamua kujikita katika shughuli ya uvuvi.

Omari, mvuvi anayeishi katika kijiji cha Mdimni, anayetumia mitumbwi midogo ya asilii, anasema siyo salama maishani na inavua samaki wachache wasioweza kujiongezea kipato kikubwa, katika ngazi ya familia na hali zao kiuchumi ni mbaya sana.

Omari anafafanua: “Nilianza kazi ya uvuvi mwaka 1985 na nilikuwa narudi nyumbani nikiwa na samaki wengi sana kwenye ndoo.”



Mvuvi Omar Kilumbi, akimueleza jambo mwanzilishi wa shirika lisilo la kiserikali Tanzania Clean Up and Conservation Initiative' (TCCI), Salum Kingungo, kuhusu tabianchi ilivyowaathiri wavuvi 400 kijijini Mdimni. **PICHA: BEATRICE PHILEMON.**

Anakiri mabadiliko ya tabianchi, yameleta madhara makubwa kwa wavuvi katika kijiji cha Mdimni, ikiwamo familia yake na mitumbwi ya asili haiwezi kufika, kutokana na kupungua kiwango cha maji na samaki baharini.

“Wavuvi wanahesabu hasara katika biashara zao, kwa sababu hakuna samaki wa kuuza kutokana na kuongezeka kwa kiwango cha maji baharini, vimbunga, upepo mkali, mawimbi ya bahari ambayo yameleta madhara katika kijiji,” anasema.

Pia, anataja madhara ya wavuvi watano kijijini wameshafariki kutokana na matumizi ya mitumbwi ya asili, huku jumla ya wavuvi 400 kijiji hicho, sasa wanaomba kusaidiwa kupata vyombo vya uvuvi vya kisasa na nyavu, ili wavue samaki na kupambana na umasikini.

“Hivi sasa wavuvi wanaishi kwa shida sana, familia zao zinashindwa hata kula chakula,” anaeleza Omari, huku akiwasilisha ombi serikalini, kupata vitendea kazi na vifaa vya kisasa kwa kazi za baharini, akitaka samaki kupatikana maeneo ya mbali.

Omari anaeleza kabla ya mabadiliko ya tabianchi, biashara ilikuwa nzuri alipovua ndoo tatu za samaki kwa kutumia mtumbwi wa asili na kumuwezesha kumpatia wastani wa Sh. 20,000 hadi Sh. 50,000.

Analalamika kwamba, sasa anaambulia robo beseni ya samaki inayompatia Sh. 5000 na ana ufafanuzi: “Hivi sasa maisha yangu yamebadilika, nina kula mlo mmoja kwa siku mimi na familia yangu.

“Wakati mwingine tunalala bila kula chakula kwa sababu fedha ninayopata kutokana na kuuza samaki ni ndogo sana na haiwezi kutosheleza mahitaji ya familia yangu,” anasema.

Inaelezwa, wavuvi wengi kijijini hivi sasa wanahangaika kutafuta fedha za kulisha familia zao, kutokana na ukosefu wa samaki na kila siku kiwango cha maji ya baharini kinazidi kuongezeka.

Hadi sasa wavuvi waliobomolewa na kuhama nyumba zao, wanafika 200, wakiwa wamekimbilia vijiji jirani, Kisemvule na Kivinje, kutafuta kazi hasa kwenye viwanda vipya vinavyojengwa na wengine kukimbilia ajira za vibarua katika mashamba ya watu, wajikimu na familia zao.

“Tunafanya kazi za vibarua kwenye mashamba ya korosho kwa mfano mkulima anakwambia ulime ekari mbili au nne, anakulipa Sh. 5000 au Sh. 2000 tu.Yaani maisha kwa ujumla ni magumu sana,” anasema.

Omari anaeleza kuna wakati wanaambulia samaki wa kula tu, huku wastani wa asilimia 80 ya wakazi wa kijiji cha Mdimni wanategemea shughuli za uvuvi.

**NGO INAYOSAIDIA**

Mwanzilishi wa shirika lisilo la Kiserikali linaloitwa Tanzania Cleanup and Conservation Initiative’ (TCCI), Salum Kingungo, anasema wameazisha kampeni ya kutoa elimu kwa wanakijiji kuhusu upandaji mikoko, athari za mabadiliko ya tabianchi na utunzaji mazingira.

Lengo kuu analitaja ni wananchi kupanda mikoko ufukweni, kupunguza kasi ya mawimbi bahari, ambayo hivi sasa yanawaletea madhara kwa wananchi, kuu ni kubomoa makazi yao.

“Hivi sasa tupo katika hatua ya kupeleka maombi kwa uongozi wa shule ( msingi na sekondari) ili kusaidia wanafunzi kujua umuhimu wa mikoko na athari za mabadiliko ya tabia nchi kwa sababu wananchi katika kijiji hiki wanakata sana miti ya mikoko,” anasema

Anasema wameamua kujikita katika kampeni hii ili kubadilisha ‘mindset’ ya watoto na wazazi wao ili wajue umuhimu wa mikoko na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

“Wakati wa utekelezaji wa kampeni hii tutaanzisha kitalu cha miche ya mikoko ambayo itakuwa inatolewa bure kwa wanafunzi na wazazi wao bure ili watu wakapande ufukweni na mpaka sasa wapo kwenye mchakato wa maandalizi ya elimu,” anasema.

Ni mradi endelevu wa upandaji miti ya mikoko katika kijiji cha Mdimni na maeneo mengine, ambayo yameanza kuathirika na mabadiliko ya tabianchi. “Mikoko inasaidia kupunguza wimbi la bahari, inasaidia mazalia ya samaki, inazuia mmonyoko wa ardhi na ni sehemu ya mazalia ya viumbe wengine kama ndege, nyoka na viumbe wengine,” anasema.

**UONGOZI WA KIJIJI**

Mwenyekiti wa kijiji cha Mdimni, Adam Ulanga anasema kuwa kijiji cha Mdimni kimeanzishwa mwaka 1971, mpaka sasa kina wakazi 1332, kati ya hao wavuvi 400 na kaya masikini ni 90.

Takriban sehemu yote ya wakazi wa kijiji hicho wanategemea mazao ya korosho, minazi embe na uvuvi ili kuongeza kipato.

“Ni kweli hivi sasa wavuvi wanaishi kwa shida, hali ya uchumi wao ni duni sana, kiasi cha kwamba wengi wameacha shughuli za uvuvi kwenda kutafuta kazi sehemu nyingine, ili wapate fedha za kulisha familia zao.

“Hawawezi kuvua samaki kwa sababu wanatumia mitumbwi ya asili ambayo haiwezi kufika sehemu za mbali baharini,” anasema.

Kutokana na changamoto hiyo, hivi sasa ameanza kuwahamasisha wavuvi kijijini hapo na kujiunga katika vikundi au vyama, ili waweze kupata mikopo au vifaa vya kisasa vya uvuvi kutoka serikalini au kwa wadau waeendelee na shughuli zao za uvuvi.

“Jumla ya wavuvi 120 wakiwamo wanawake na wanaume tayari wamejiunga katika kikundi kinachoitwa ‘Tangu Asili’ kulingana na kazi wanazozifanya,” anasema

Anasema anavyovihitaji sasa, kutoka serikalini na wadau wengine ni kupata mafunzo, jinsi ya kuanzisha vyama vya ushirika au kuweka na kukopa, uendeshaji, elimu ya ujasiriamali, vifaa bora vya uvuvi na mkopo, ili wabadilishe maisha yao, wanufaike na biashara ya uvuvi.

Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filberto Sanga, alipozungumza na Nipashe, anafafanua kuhusu hali ya wavuvi wilayani yameshaathiri maeneo mengi ya Mkuranga, hasa katika bonde linalounganisha vijiji vya Nasibugani na Mavunja.



Wavuvi kijijini Mdimni, wakielezea walivyoathiriwa na mabadiliko tabianchi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

## TANESCO na ujenzi wa nyumba zetu






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

OKTOBA 13, mwaka huu, ni siku ambayo mkazi wa Pugu Stesheni mkoani Dar es Salaam, Edward Katemi hataisahau na itaendelea kukaa kichwani na katika kumbukumbu zake zingine, kama siku mbaya kupata kutokea katika historia ya maisha yake.

Ni siku ambayo alipoteza sehemu kubwa ya familia yake kutokana na ajali ya moto, iliyoangamiza roho na nyoyo za mkewe Jackline Frank, wanawe Edwin, Edison na Ivan na mdogo wake, Esther.

Inauma zaidi, kwamba alishuhudia janga hilo huku akishindwa kuwaokoa marehemu hao, baada ya kushindwa kupumua kutokana na moshi mkubwa uliogubika vyumba walimokuwa wakati moto ukiendelea kupamba.

Ilidaiwa kuwa chanzo ni umeme. Kwamba ulikatika na uliporejea, ukaathiri swichi kubwa na mlipuko kutokea eneo hilo na kushika nyumba nzima. Kwa mujibu wa maelezo ya Katemi, akiwa getini akipiga honi afunguliwe, umeme ulirudi na kukatika nyumbani kwake tu na kufuatiwa na cheche na hatimaye moto huo.

Ingawa mpaka safu hii inaandikwa hakuna taarifa rasmi iliyotolewa ama na Jeshi la Zimamoto au Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) hata kufanya Mzee Amos Jeremia, baba wa Katemi kumwachia yote Mungu, chanzo kitabaki kuwa tatizo la umeme.

Ni janga kubwa linalostahili rambirambi na pole nyingi, si tu kutoka kwa ndugu, jamaa na marafiki, lakini hata Tanesco ambayo bidhaa yake ndiyo bado inaaminika kuwa chanzo cha maafa haya.

Ningetarajia kusikia Tanesco wamekwenda kuhani lakini hata kushirki maziko ya wanandugu hao, yaliyofanyika Buchosa, mkoani Mwanza, lakini hilo halikufanyika, sababu wanazijua wenyewe.

Pengine hatua ya Mzee Jeremia kumwachia Mungu ilitokana na kuamini kwamba, hakuna kitakachofanyika kuwafuta machozi au hata kurejesha roho za wapendwa wao. Mara nyingi kama si zote, Watanzania ni wepesi wa kukata tama na kumwachia Mungu mara wapatapo matatizo.

Bila shaka ni hulka nzuri isiyotaka mtafaruku na kuamini kwamba, hakukuwapo makusudi katika kutokea ajali hiyo, ingawa wakati mwingine kukatika umeme ama husababishwa na ubovu wa miundombinu au uzembe wa wasimamizi wake.

Mara kadhaa umeme umekatika katika majengo mbalimbali na kurudi kwa nguvu bila hadhari yoyote, na matokeo yake ama vitu kuharibika au kuungua na kuwa sababishia hasara wateja, lakini nao wamekuwa wakimwachia Mungu, kutokana na urasimu mbaya wa kudai haki, endapo wangefanya hivyo.

Si siri, kuwa vifaa vingi vitumiavyo nishati ya umeme majumbani vilishakumbwa na matatizo hayo na wamiliki kubaki kimya na kuingia gharama za kuvirekebisha au hata kuvitupa kabisa.

Tanesco kwa kujua kuwa ni muhali kwao, wamekuwa kimya bila kuwambia kinagaubaga wateja wao, kuwa linapotokea hilo wafanye nini.

Iwapo vifaa tu hilo halifanyiki na pia kuchelea kufuatilia madai mpaka walipwe, sembuse maisha ya watu watano? Ni lini sasa serikali kupitia Tanesco, itaweka utaratibu wa kuwajibishana ithibitishwapo kuwa chanzo ni umeme?

Kwa upande mwingine, tukiangalia kiini cha vifo vya watu hao wa familia ya Katemi, tunabaini vilitokana na kukosa hewa na si moto kuwaunguza. Waokozi walifanikiwa kuwatoa bila ya majeraha ya moto huku wakipumua kwa shida, kutokana na kuzidiwa na moshi.

Tunajifunza nini? Ujenzi wa nyumba zetu. Siku hizi kuna ujenzi ambao hauzingatii afya. Mtu anajenga nyumba na kuweka madirisha ya vioo vinavyofunga gubigubi na kusahau kuwapo mwanya wa kutolea au kuingizia hewa. Vioo vinafunga madirisha huku kukiwa hakuna kiyoyozi.

Endapo nyumba ya aina hiyo itakumbwa na janga la moto kama hivi, moshi utakosa pa kutokea na hasa inapokuwa ni usiku na vioo vimefungwa; matokeo yake ni walioko ndani kukosa hewa na kuvuta moshi na kusababisha majanga kama hayo.

Sijachunguza nyumba ya Katemi, lakini yawezekana kuwa katika mfumo huo. Poleni sana wafiwa.

UCHUMI

# Geneva; jiji linaloongoza kulipa mshahara mkubwa duniani kote

- Kima cha chini Sh. milioni tisa kasoro
- Wenye migahawa walia 'tutawezaje?'
- Mshahara safi, gharama nazo...mmh!
- Wakazi 600,000 waombaji wa vyakula



Wakazi wasio na uwezo jijini Geneva, wakiwa kwenye foleni ya kupatiwa msaada wa chakula. **PICHA: MTANDAO.**

**Geneva, Uswisi**

GENEVA, mji mkuu wa Uswisi ni makao makuu ya baadhi mashirika makubwa na kunatajwa kuwa ngome ya watu tajiri zadi duniani. Lakini unajua, kuna baadhi ya , wakazi wake wanapewa msaada wa chakula?

Hapo ni makao makuu ya benki kubwa za sekta binafsi, mashirika ya Umoja wa Mataifa na majumba ya mnada ya Sotheby na Christie, ambayo kila mara huuza mawe ya thamani kwa bei ghali sana.

Ni wiki kadhaa iliyopita, mji huo ulianza kutekeleza kiwango cha juu zaidi cha malipo ya chini ya mshahara wa kila mwezi duniani, kujibu matakwa ya watu katika kura ya maoni ya mwishoni mwa mwezi Septemba mwaka huu .

Kiwango kipya cha malipo ya faranga 23 za Uswisi - ambacho ni sawa na Euro19, dola 25 au paundi 22 - kitawapatia watu kiwango cha chini zaidi cha mshahara kuwa Euro 3,350 sawa na Sh.8, 999,050.

**KINACHOFANYIKA**

Mshahara wa chini wa Geneva umeidhinishwa kuwa sheria si kwa sababu ni hatua iliyowekwa na serikali, bali pendekezo mjini Geneva uitwao"mpango wa wananchi".

Walikusanya saini nyingi kutaka suala hilo lipigiwe kura ya maoni na hadi kufika Septemba 27, asilimia 58 ya wapiga kura walijitokeza.

Utaratibu uliopo Uswizi ni kinachoitwa 'demokrasia ya moja kwa moja' ukimaanisha kwamba wapiga kura wana uamuzi wa mwisho, hali inayofanya kiwango hicho cha chini cha lazima.

Hadi sasa kuna hofu kwa mishahara ya migahawa, kumudu viwango vipya.

Mara nyingi, raia wa Uswisi hupiga kura kwa makini na linapokuja suala la matumizi ya fedha za umma. Siku hiyo hiyo pia waliunga mkono likizo ya wiki mbili ya uzazi kwa mzazi wa kiume, ikiwa na malipo.

Mdau Charly Hernandez, hatua zilizopo ni dalili njema, akiwa na ufafanuzi:"Walipigia kura, na hilo limenifurahisha sana. Tuna demokrasia ya moja kwa moja na hilo ni jambo zuri sana, lakini kile watu wasichokijua ni kwamba juhudi nyingi za kiraia hupuuzwa.

"Ni vyema kwamba mambo yameanza kubadilika na baadhi ya vitu vinaidhinishwa, kwa hiyo naamini mambo yanazidi kuimarika ... japo kwa mwendo wa polepole, lakini ndio kasi ya Uswizi," anasema.

Mpango huo utazihitaji kampuni zilizo na makao yake nchini Uswisi kuwajibika kisheria na kifedha, itakapotokea ukiukwaji wa haki za kibinadamu katika hatua za utendaji wa kampuni hizo kokote duniani.

**KULIKONI HIVYO?**

Mji huo wa nchini Uswisi, huenda ukawa na utajiri mkubwa kwa maelfu ya wafanyakazi wa hoteli, wahudumu wa migahawa, wanaotoa huduma za usafi na wafanyakazi wa saluni wanaojitahidi kumudu gharama kubwa ya maisha.

Wakati nchi ya Uswisi ilipoweka amri ya kutotoka nje. hadi Machi mwaka huu kudhibiti kuenea virusi vya corona, kulishuhudiwa milolongo mirefu ya watu waliosubiri kupokea msaada wa chakula jijini Geneva.

Pia, kunatajwa utoaji chakula ilikuwa suala lililokuwapo hata kabla ya janga corona.

Charly Hernandez, kutoka shirika la msaada Colis du Coeur, ambalo ndio linagawa chakula kwa umma kila wiki katika maeneo ya katikati ya mji. Anasema wanawake ndio wanaonekana zaidi katika foleni ya kupata chakula, wakiwa na watoto wao.

Inaelezwa kitakwimu, ndani ya jiji Geneva lenye wastani wa wakazi milioni 8.5, walio hohehahe kudai msaada kama wa chakula jumla yao ni wastani wa 600,000.

**MAKALI YA MAISHA**

Je, ujira wa wa Faranga 4,000 kwa mwezi unatosha? Huenda ikaonekana pesa nyingi, iwapo tu huishi jijioni Geneva, anatamka maksi ajitabulishae kwa jina, Charly.

"Chumba kimoja kinakodishwa kwa faranga 1,000 kwa mwezi, ikiwa utafanikiwa kununua chakula kwa faranga 500 kwa mwezi basi wewe ni hodari kwa kubana matumizi, bima ya afya ni 550 kwa mwezi kwa kila mtu. Ukiwa na mke na watoto wawili niambie utasalia na nini."

> **"Mwisho wa mwezi mifuko yao inasalia bila kitu," anasema mkazi aitwae Ingrid anaendelea: "Migahawa (ya chakula) imesaidia sana, kwa sababu watapata ahueni japo kwa wiki moja."**

Inaelezwa, gharama ya maisha jijini Geneva iko juu sana na wafanya kazi wengi wanajikamua kuishi katika mazingira magumu

Sheria mpya ya malipo inayoweka kiwango cha chini cha mshahara, inadaiwa itawasaidia wengi, ambao wanaishi kijanja kula vyakula vya bei nafuu migahawani.

"Mwisho wa mwezi mifuko yao inasalia bila kitu," anasema mkazi aitwae Ingrid anaendelea: "Migahawa (ya chakula) imesaidia sana, kwa sababu watapata ahueni japo kwa wiki moja."

Hata baadhi ya watu wanaojitolea kufanya kazi kama Laura, ambaye ni muuguzi, anaona gharama ya maisha jijini Geneva iko juu sana na hawezi kupata nyumba nzuri ya kuishi mjini hupo.

"Ningelikuwa naishi katika chumba kimoja kidogo. Sasa bado naishi na wazazi wangu. Nina miaka 26," anasema.

**MLIPAJI NANI?**

Kutokana na mwongozo mpya wa malipo, biashara zinazowalipa wafanyakazi chini ya wastani wa Faranga 23 kwa saa ya sasa, watalazimika kuwaongezea. Hatua ya kutekeleza malipo hayo mapya.

Vincent Subilia kutoka Chama cha Wafanyabiashara wa Geneva, anaeleza kwa hofu kwamba, hiyo inakuja ikiwa ni katikati ya janga corona, iliyochangia kushuka faida na kuna athari kubwa

"Hoteli na migahawa tayari zinakabiliwa na changamoto kadhaa kutokana na janga hili," anasema, kwa ufafanuzi kwamb a ni hali huenda ikasambaratisha sekta hizo.

Mmiliki wa migahawa, Stefano Fanari, ana ufafanuzi kwamba haoni namna atamudu malipo yanayotakiwa kwa watalaamu kama mpishi mkuu, ambaye marupurupu yake ya mwezi ni kati ya faranga 5,000 na 6,000.

"Nitawezaje kuendelea wakati natakiwa kuwalipa waosha vyombo kiasi hicho cha fedha?" anaelejeza hofu yake, akiwa na maswali yasiyo na majibu kwamba:

"Je nipunguze saa za kufanya kazi? Msinielewe vibaya, Sipingi suala la wao kulipwa (fedha) 4,000 kwa mwezi. Lakini kwa hali ilivyo, hatuwezi kumudu malipo hayo. Nimejitolea, Nafanya kazi hapa kwa saa 12 kwa siku. Nifanye nini?"





Rais Dk. John Magufuli akikagua gwaride la heshima lililoandaliwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), kabla ya kuapishwa kuwa Rais wa Awamu ya Tano katika muhula wa pili, uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Sendiga ataka ushirikiano kwa Rais John Magufuli

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MGOMBEA urais kupitia Chama cha ADC, kwenye uchaguzi mkuu 2020, uliofanyika Oktoba 28, Queen Sendiga, ameviomba vyama vya siasa kumpa ushirikiano Rais John Magufuli, ili aendelee kutatua kero za Watanzania.

Sendika, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza kwenye mahafali ya kidato cha nne ya Shule ya Sekondari ya Fountain Gate ya jijini Dodoma.

Akizungumza na wazazi na wanafunzi wa shule hiyo, aliwaomba viongozi wa vyama vya siasa kumpa ushirikiano Rais Magufuli, ili atatue kero mbalimbali zinazowakabili Watanzania katika maeneo mengi nchini.

"Ninawaomba viongozi wa vyama vya siasa wezangu, kumpa ushirikiano mkubwa Rais, Dk. Magufuli katika kutatua kero za Watanzania, mimi nilipokuwa kwenye kampeni nimejionea mwenyewe jinsi wananchi wanavyokabiliana na kero mbalimbali," alisema.

"Nimetembea karibu mikoa 20 na wilaya zipatazo 140, na nimekuta kuna kero nyingi zinazowagusa Watanzania walio wengi zikiwamo huduma za elimu, maji, kilimo, ufugaji, afya na miundombinu ya barabara," alisema.

Alisema: "Ni muhimu sasa kuachana na mambo ya siasa badala yake tushikamane kwa pamoja na Rais aliyepo madarakani, tuungane kufanya kazi kwa pamoja."

Akizungumzia kwa upande wa wanafunzi, aliwataka kujikita kwenye elimu zaidi ili wawe viongozi wenye maadili kwa ajili ya maslahi ya maendeleo ya nchi.

Naye Mbunge mteule wa Jimbo la Mbagala mkoani Dar es Salaam, Abdalah Chaurembo, aliwaomba wazazi na walezi kuhakikisha wanashirikiana na walimu ili watoto wafanye vizuri kitaaluma na kimichezo.

Aidha, aliwataka wanafunzi hao kutoridhika na hatua waliyofikia ya kidato cha nne, badala yake wajipange kwa safari nyingine ya juu ili kufikia malengo waliyojiwekea.

Aliipongeza shule hiyo kwa hatua yake ya kuisaidia serikali kwa kutoa ajira kwa Watanzania kutoa ajira.

# Onyo matumizi mabaya ya vitambulisho vya machinga

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISA masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, amesema kuwa vitambulisho vya machinga havikutolewa kuwa sehemu ya kuvunja sheria kwa kufanya biashara kwa kupanga bidhaa zao kwenye maeneo yasiyoruhusiwa.

Yuna alisema hayo alipokuwa akizungumza na viongozi wa machinga alipofanya ziara ya kukagua maeneo mbalimbali yanayotumiwa na wafanyabiashara.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara hao kuhakikisha hawavuki mipaka na kuvunja sheria hata kama wana vitambulisho hivyo.

Alisema kuwa na kitambulisho cha machinga siyo jawabu la kupata uhuru wa kufanya biashara kila eneo, bila utaratibu na kuvunja sheria za halmashauri ya jiji na kuzingatia maelekezo yaliyotolewa yanazingatiwa.

Pia, aliwataka watumiaji wa masoko ndani ya Jiji kujenga utamaduni wa kununua mahitaji yao kwenye maeneo yaliyo rasmi, ili kuepukana na hatari zinazoweza kutokea ikiwamo za kiafya.

Vile vile, alisema kuwa kwenye maeneo ambayo yapo rasmi wapo wataalamu wa kiafya, ambao wamekuwa wakisimamia ubora wa viwango na mpangilio wa bidhaa zote zinazouzwa kwa ajili ya mahitaji.

Akizungumza kwa niaba ya viongozi, Makamu Mwenyekiti wa Machinga Wilaya ya Dodoma, Bruno Mponzi, alisema kuchaguliwa kwa Rais John Magufuli, ni matumaini yao kufanya biashara zao kutoka katika hatua ya umachinga hadi wafanyabiashara wakubwa.

"Sisi machinga tunampongeza Rais Magufuli, kwa kuchaguliwa kuongoza awamu hii ya pili, hivyo ni matumaini yetu kwenye utendaji wake kama tulivyoshuhudia tutafanikiwa kwa kiasi kikubwa na kufikia hatua ya ushindani wa masoko ya nje," alisema.

Hata hivyo, aliwataka machinga kutoa ushirikiano kwa Halmashauri ya Jiji ili kuvitumia vitambulisho walivyonavyo na kutovunja sheria na kanuni kam a walivyoelekezwa.

# Walima karanga wapatiwa mbinu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKULIMA wa karanga, wametakiwa kulipa kipaumbele zao hilo kutokana na kustahimili hali ya hewa ya Mkoa wa Dodoma.

Ushauri huo ulitolewa jana na aliyekuwa Ofisa Kilimo mstaafu wa Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, Aidan Chaula, wakati wa mafunzo ya kilimo cha karanga yaliyoendeshwa kwa ushirikiano wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, (TARI), Naliendele na Taasisi wa kudhibiti ubora wa mbegu nchini (TOSCHI).

Chaula alisema karanga ni miongoni mwa mazao yanayostawi kwa wingi mkoani Dodoma na kama kilimo hicho kitatiliwa maanani, kitaongeza uzalishaji. "Karanga ni zao lenye tija kubwa, wakulima wanapaswa kuchangamkia fursa hiyo," alisema Chaula.

Akitolea mfano karanga aina ya mnanje na mangaka alisema zinastawi vizuri katika mkoa wa Dodoma, hivyo ni vema wakulima wa zao hilo jijini hapa kutumia mbegu hizo.

"Mwaka huu nimefanikiwa kuvuna magunia 200 kutokana na kutumia mbegu hizo zilizoainishwa," alisema Chaula.

Hata hivyo, alisisitiza kuwa karanga alizopanda mbegu zake zilipatikana katika kituo cha utafiti cha Naliendele kilichopo mkoani Mtwara.

Alifafanua kuwa anasisitiza wakulima walime zao la karanga kwa sababu tokea enzi wakazi wa Dodoma walikuwa wakihimizwa kupanda karanga, kwa sababu hali ya hewa inaruhusu zao hilo kustawi kwa wingi, ikiwamo kutoa mavuno mengi.

Aliongeza kuwa kukiwa na uhakika wa uzalishaji mbegu unaoendana na mazingira na mbegu hizo zikapatikana kwa wakati, wakulima watapata mbegu zinazofaa na kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

"Mkulima akipanda Desemba mwishoni anavuna mwezi Aprili, ni karanga inayozaa sana na kwenye shina moja unaweza kupata punje zaidi ya 100

zile kwenye maganda na ndani yake unaweza kupata punje tatu hadi nne," alisema Chaula.

Alisema karanga aina ya naliendele nayo ina siku 100 inazaa sana na inatafutwa sokoni kwani haina mafuta mengi na hutumika sana katika kutengeneza siagi ya karanga.

"Naliendele inakuwa haraka sana ndani ya mwezi mmoja inaanza kutoa maua na hata kama mvua ndogo unaweza kuvuna mazao mengi," alisema.

Alisema karanga aina ya mnanje ni zenye punje kubwa zina rangi nyekundu na imekuwa ikipendwa sana kutokana na kuwa na madini ya zink, calcium na magnesium ambayo ni nzuri sana kwa lishe na kuongeza kuwa nnanje inatumia siku 120 tokea kupandwa hadi kuvuna.

Kwa upande wake, Ofisa Mdhibiti Ubora wa Mbegu kutoka TOSCHI, Zella Mwakemwa, alisema wanahakikisha wakulima wanapata mbegu bora kwa kuzingatia sheria.

"Tunahakikisha mbegu zote zinakuwa na ubora na kuwa na tija na kufanya ukaguzi kwa wazalishaji wa mbegu," alisema.

Kaimu Ofisa Kilimo Wilaya ya Chamwino, Anastazia Pascal, aliwataka wakulima wa Chamwino kutumia fursa ya kilimo cha karanga.



# Wahitimu vyuo wajitolea kufundisha bure

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

VIJANA 41 waliohitimu vyuo vikuu nchini, wameamua kuungana na kufanya kazi ya kujitolea bila malipo kufundisha shule za sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Kupitia umoja wao uitwao COFAPS, vijana hao wameanzisha kampeni hiyo baada ya kuona shule nyingi hasa za pembezoni zikifanya vibaya kwenye matokeo ya kidato cha pili na cha nne, hivyo kuamua kuja na mwarobaini huo.

Kaimu Katibu wa Umoja huo, Carol Mirambo, alisema kwa sasa vijana hao wametawanyika katika shule mbalimbali ndani ya halmashauri hiyo wakiendelea na jukumu la kufundisha kwa kujitolea.

Alisema COFAPS ilianzishwa mwaka 2017 ikiwa na vijana saba pekee ambao waliamua kujiunga kwa pamoja baada ya kuhitimu vyuo vikuu na kukosa ajira ili kuwasaidia wadogo zao.

"Licha ya kukosa ajira baada ya kuhitimu elimu ya vyuo vikuu, tuliamua kujiunga vijana 41 kufundisha wanafunzi wa kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita," alisema Mirambo.

Hata hivyo, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, ambaye ni Ofisa Elimu Sekondari, Aliko Mbuba, alisema vijana hao wamekuwa msaada mkubwa katika kupunguza uhaba wa walimu shuleni.

Alisema vijana hao wamesaidia kuziba pengo la walimu hususani masomo ya sayansi na hesabu, hivyo kuwawezesha wanafunzi kumaliza silabasi za masomo mapema kulinganisha na ilivyokuwa awali. Uhaba wa walimu ulichangia wanafunzi kutomaliza baadhi ya silabasi.

"Mbali na kupewa kibali cha kufika kwenye kata zote, vijana hawa wamekuwa msaada mkubwa kwa wanafunzi hasa madarasa yenye mitihani ya taifa ambayo kwa ujumla wake imeongeza ufaulu huku wakiwa na tumaini la kupata ajira serikalini," alisema Mbuba.

Licha ya shule za sekondari wilayani humo, kujitosheleza kwa masomo ya sanaa na biashara halmashauri hiyo ina upungufu wa takribani walimu 88 wa masomo ya sayansi.

Alisema halmashauri ilipokea kwa mikono miwili ombi la vijana hao kufika kwenye kata zote 28 za wilaya hiyo baada ya kuona matunda.



Wakazi wa Kijiji cha Sangambi, katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, mkoani Mbeya, wakiendelea na shughuli za uchenjuaji madini kwa kutumia kemikali aina ya zebaki, karibu na makazi ya watu jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# RC ataka uchangiaji miradi ya maendeleo

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA.

LICHA ya serikali kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maendeleo hasa sekta ya afya, wananchi nao wametakiwa kuchangia fedha na nguvu zao, ili miradi hiyo itekelezwe kwa ufanisi mkubwa.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliyasema hayo juzi wakati akikagua miradi mikubwa mitatu ya ujenzi wa miundombinu ya afya iliyo ndani ya Jiji la Mbeya.

Miradi iliyokaguliwa na mkuu huyo wa mkoa ni jengo jipya la ghorofa tano linalojengwa katika Hospitali ya Rufani ya Wazazi Meta, upanuzi wa Hospitali ya Jiji la Mbeya ya Igawilo na ujenzi wa wodi la mama na mtoto katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya.

Chalamila alisema serikali imejitahidi kuwekeza kwenye sekta ya afya kwa sababu ni eneo ambalo linagusa maisha ya wananchi kwa kiasi kikubwa, hivyo jitihada zao zinahitajika ili kukamilisha miradi hiyo kwa wakati.

Akizungumza na wananchi baada ya kukagua miradi hiyo, Chalamila alisema ili miradi hiyo iwe na umiliki wa wananchi moja kwa moja, wananchi pia wanapaswa kuchangia utekelezaji wa miradi hiyo.

"Serikali imetuletea miradi hii mikubwa kwa faida yetu, hivyo ili miradi hii iwe na umiliki wetu na ili tuwe na uchungu nayo, ni lazima wananchi pia tuchangie utekelezaji wake," alisema Chalamila.

Msimamizi wa mradi wa jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya ambaye pia ndiye Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Gloria Mbwilo, alisema mradi huo ukikamilika utawasaidia wananchi kupata huduma nzuri na kwa ufanisi mkubwa.

"Kwa sasa jengo la kutolea huduma ya mama na mtoto katika hospitali hii ni dogo ambalo halikidhi mahitaji kulingana na idadi ya wateja wetu, hivyo jengo hili likikamilika wananchi wengi zaidi watapata huduma hapa na itatusaidia hata sisi watoa huduma kuwahudumia vizuri wananchi," alisema Dk. Mbwilo.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, alionya kuwa fedha hizo zinazotolewa na serikali kwa ajili ya kutekeleza miradi, inapaswa kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa na sio vinginevyo.

"Fedha hizi zinazotolewa na serikali kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni sawa na maji ya betri. Mtu yeyote akijaribu kuyanywa lazima yatamdhuru, hivyo ni lazima fedha hizi ziheshimiwe na kufanya kazi iliyolengwa," alisema Ntinika.

Serikali katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, imeboresha sekta ya afya kwa kujenga miundombinu mipya na kuboresha ya zamani. Katika Jiji la Mbeya, imejenga vituo vipya vya afya na hospitali pamoja na kuboresha hospitali kadhaa zilizopo.

## Mila potofu chanzo ukatili wa kijinsia

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MILA na desturi potofu zimetajwa kuwa ni miongoni mwa sababu zinazochochea vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, hali inayosababisha makundi hayo kunyimwa haki za msingi.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa Vituo vya Taarifa na Maarifa ambavyo vimejingewa uwezo na TGNP Mtandao juu ya masuala ya uongozi na upangaji wa bajeti wenye mlengo wa kijinsia, Flora Mlowezi.

Alisema vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto na wanawake hususani katika maeneo ya pembezoni bado vinachagizwa na masuala ya mila potofu ambazo zimepitwa na wakati, hivyo kuwanyima wanawake haki na mahitaji yao ya msingi.

Mlowezi alisema hali hiyo inasababisha kundi la wanawake na watoto kujiona sio sehemu ya jamii husika hali inayosababisha makundi hayo kuachwa nyuma katika masuala mbalimbali ikiwamo kushirikishwa kwenye kujadili na kuamua ajenda za maendeleo.

"Wahanga (waathirika) wa masuala hayo ni wanawake na watoto kwa kuwa wanafanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia, mimba za utotoni, vipigo, kuporwa haki ya kumiliki mali, kubebeshwa majukumu makubwa, kutopewa nafasi ya uongozi kwa kisingizio cha jinsia," alisema.

Alisema kutokana na changamoto hizo wadau mbalimbali wa masuala ya kijinsia ikiwamo TGNP-Mtandao wameona kuna umuhimu wa kutoa elimu kwa jamii kuachana na mitazamo hadi kuhusu masuala ya jinsia.

Alisema vituo vya taarifa na maarifa katika kata hizo ambavyo vinawezeshwa na TGNP-Mtandao vimefanya kazi kubwa ya kutoa elimu na kuwa vuguvugu la mapinduzi katika harakati za kuleta mabadiliko kifikra kwa jamii hizo ambazo awali zilikuwa zimejikita na mfumo dume.

Naye Lydia Mwakalinga, alisema mafunzo hayo yatakuwa chachu kwa wanawake kuwasilisha changamoto zao kwenye vikao vya maamuzi bila ya uoga.

Alisema mafunzo hayo yanawaandaa wanawake na vijana kuwa viongozi bora katika kuwasilisha vikwazo vinavyokabili makundi hayo.

# Amani yaanza kurejea kisiwani Pemba

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

HALI ya amani na utulivu imeanza kurejea Kisiwani Pemba, huku baadhi ya wafanyabiashara katika mitaa mbalimbali ya mji wa Chakechake wakiendelea na biashara zao.

Tangu Oktoba 27, mwaka huu, wafanyabiashara walisita kufanya biashara zao kutokana na baadhi ya vitendo vya uvunjifu wa amani vilivyojitokeza kisiwani humo, lakini vyombo vya ulinzi na usalama vilifanikiwa kuvidhibiti vitendo hivyo.

Katika soko la matunda la mjini Chakechake, baadhi ya wafanyabiashara wameanza kurejea na kufanya shughuli zao ingawa huduma za usafiri wa magari ya abiria hazijarejea jambo ambalo linawanyima wafanyakazi hususan wanaoishi nje ya mji, kushindwa kufika kazini mwao.

Wakizungumza na Nipashe juzi, baadhi ya wafanyabiashara hao, walisema wamekuwa wasiwasi kwamba kuendelea kuwapo katika biashara zao kunaweza kukatokea machafuko na kupoteza mitaji yao.

"Biashara zangu hapa sokoni nimeanza kufanya leo (juzi), hivyo nawaomba wananchi kudumisha amani ya nchi, kuwa na upendo na ushirikiano ili tusonge mbele kimaendeleo," alisema Ali Juma, mfanyabiashara katika soko la Chakechake.

Hata hivyo, baadhi ya bidhaa zimepanda bei kutokana na upungufu wake na kuwapo kwa wafanyabiashara wachache sokoni hapo.

Kilo moja ya vitunguu maji ni Sh. 2,000 badala ya Sh. 1000 iliyokuwa ikiuzwa kabla ya uchaguzi mkuu wakati kisado kimoja cha nyanya ni Sh. 5,000 badala ya Sh. 2,500 hapo awali.

"Tumelazimika kuuza bidhaa kwa bei hii kutokana na kwamba hizi bidhaa hapa kwa muda huu baadhi yetu hawafungui biashara kutokana na woga tulio nao hii nchi tunaona haijatulia," alisema Muhammed Khamis, mfanyabiashara mwingine sokoni hapo.

Baadhi ya wafanyakazi wa taasisi za serikali wameshinda kufika ofisini kutokana na shida ya usafiri wa abiria (daladala) iliyoko kisiwani Pemba.

Dereva wa gari la abiria kutoka Kiuyu, Micheweni, Hamad Ali, alisema wamelazimika kusitisha kufanya safari zao kutoka Micheweni hadi Chakechake kwa sababu hakuna abiria ili kuepuka hasara.



Mwenyekiti wa Baraza la Vijana Zanzibar, Khamis Rashid Kheir (aliyevaa koti), akizungumza na waandishi wa habari, alipotembelea wafanyabiashara wa soko la mboga la Mombasa, Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# UWT yampongeza Mwinyi kwa ushindi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UMOJA wa Wanawake wa Tanzania (UWT) wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kusini Unguja, umetoa salamu za pongezi kwa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa kuiongoza Zanzibar kwa kipindi cha miaka mitano.

Pongezi hizo zilitolewa jana na Kaimu Katibu wa UWT Mkoa wa Kusini Unguja, Asha Mzee Omar, ofisini kwake Dunga, Wilaya ya Kati wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari, kutokana na uchaguzi mkuu uliomalizika hivi karibuni na CCM kushinda kwa kishindo.

Alisema wanawake wa mkoa huo watatoa ushirikiano kuhakikisha malengo ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025 yanafikiwa kwa miaka mitano ijayo.

Kuchaguliwa kwa kiongozi huyo kwa kura nyingi na kupata asilimia kubwa ya ushindi kwa kishindo ya 76.27, alisema inaonyesha dhahiri kuwa wanachama wa CCM na wananchi kwa ujumla wana imani kubwa kwa kumchagua kiongozi ambaye ni jemedari.

Pia alisema Wazanzibari waliamua kuchagua kazi, historia, amani, haki, usawa na maendeleo na wameona mwangaza wa upatikanaji wake ni kupitia Dk. Mwinyi kutokana na kuridhishwa na sera za chama chake na ilani ya CCM.

Alisema ni imani ya wanachama wa CCM na wananchi kwa ujumla kutokana na uadilifu, uzalendo, uchapakazi, ufuatiliaji alionao amejitolea kwa dhati kuwaletea maendeleo Wazanzibari.

"Tumemwomba Mungu ampe nguvu, subira na kila la heri katika kusimamia utekelezaji wa majukumu yake Rais Dk. Mwinyi," alisema.

# Rushwa chanzo kushamiri udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

LICHA ya serikali kuunda mamlaka maalum ya kupambana na rushwa, ili kudhibiti vitendo vya ufisadi na uhujumu wa uchumi, baadhi ya familia watoto wao waliodhalilishwa wamekuwa wakipokea rushwa ili kesi hizo zisisonge mbele.

Akizungumza jana na Nipashe, mama mmoja ambaye mtoto wake alibakwa (jina linahifadhiwa), alisema kesi ya mtoto wake imeshindwa kufikishwa mahakamani kutokana na baba wa mtoto huyo kupokea rushwa ya fedha kutoka familia ya mdhalilishaji.

Alieleza masikitiko yake ya kwamba baba wa mtoto wake aliamua kupokea fedha bila kumshirikisha yeye na wala kumpa taarifa.

"Kipindi ambacho mtoto wangu alibakwa, mimi nilikuwa na ujauzito, hivyo nilikuwa siwezi kuhangaika, nikamwachia kufuatilia kesi hiyo polisi. Baada ya kujifungua nikafuatilia kesi ya mtoto wangu ili kujua ilipofikia nikapata taarifa kuwa kesi imeshafutwa baada ya familia ya aliyedhalilishwa na mdhalilishaji kukubaliana na kuimaliza kesi katika ngazi ya kifamilia bila mimi kushirikishwa," alisema.

Aidha, mama huyo alisema baba wa mtoto wake alifanya uamuzi huo kutokana na muhali kwa sababu mdhalilishaji ni mtu wa karibu wa familia.

Naye mjumbe wa kamati ya kupambana na vitendo vya udhalilishaji, Bimkubwa Said, alisema bado muhali umekuwa ukirejesha nyuma katika mapambano ya vitendo hivyo.

Alisema baadhi ya wazazi wamekuwa wakizimaliza kesi za udhalilishaji katika ngazi za familia ama kwa kulipana fidia au watoto waliobakwa ambao ni zaidi ya miaka 15 huwafungisha ndoa.

Bimkubwa alisema hufanya uamuzi huo kwa sababu wadhalilishaji huwa ni watu wa karibu katika familia ya mtoto aliyedhalilishwa, hivyo huona aibu watuhumiwa kuwafikisha katika vyombo vya sheria.

Aidha, alisema baadhi ya askari wa Jeshi la Polisi huwa wanachangia kuwasuluhisha familia za mdhalilishaji na aliyedhalilishwa na kesi hizo kushindwa kufikishwa mahakamani.

"Kuna kesi moja ambayo naifahamu ilifikishwa katika kituo kimoja cha polisi, lakini askari polisi walizishawishi familia za mdhalilishaji na aliyedhalilishwa kumalizana na hatimaye kesi hiyo kushindwa kufikishwa mahakamani kwa sababu ya muhali maana aliyedhalilisha na aliyedhalilishwa ni baba mdogo kwa baba mkubwa," alisema.

Mjumbe huyo aliwataka wazazi na wale kuachana na muhali kwa kesi za udhalilishaji na badala yake kesi hizo kuzifikisha katika vyombo vya sheria ili kupatiwa hukumu.

Hata hivyo aliitaka jamii kushirikiana katika kutokomeza vitendo hivyo na wanapohitajika kutoa ushahidi mahakamani wawe mstari wa mbele ili washtakiwa wa kesi hizo kupatiwa hukumu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, Awadhi Juma Haji, aliwataka wananchi wanapoona kuna harufu ya rushwa katika vitendo vya udhalilishaji kutokaa kimya na badala yake kuripoti katika sehemu husika.

Kamanda alisema iwapo jamii haitakuwa tayari kupambana na udhalilishaji, vitendo hivyo havitamalizika, hivyo ni vyema kuungana kuvitokomeza.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA NA MASHAMBA

**MATHEMATICS TUITION.** Mlete kijana wako tufuatilie msingi wake wa hisabati hadi pale shida ilipoanzia na kuanza kuujenga tena upya. Wahusika ni kuanzia darasa la tano hadi kidato cha sita.Tuitions za majumbani zinapatikana pia. Tupo Bunju Mwisho Dsm. Simu 0655.0754 617987 na 0782 461858

NIPASHE NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE NASI
KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA VYETI



**THOMAS D. NYABIRI** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne chenye index namba S.4467/0079 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia ST. JOSEPH SOGA BOYS SEKONDARI mwaka 2017. Cheti cha kuzaliwa cha 08/05/2000. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya Polisi: DOD/DOD/RB/775964/2020**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**STEVEN ALFRED SHARRA**
Anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0110/00128/1995 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ILBORU-ARUSHA mwaka 1995,yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa DAR/KIJ/RB/780334/2020**

## TANGAZO LA KUPOTELEWA NA PASIPOTI YA KUSAFIRIA



**Omari Mabala Karanga**
Anatangaza kupotelewa na Pasipoti ya kusafiria iliyokwisha muda wake yenye namba AB290298 ailiyoipata ofisi ya uhamiaji makao bara makuu (PCO, Dar es salaam).
Kwa yeyote atakae iona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu, au awasiliane na Omari Mabala Karanga kwa simu namba 0765796146.
**RB Namba SHY/RB, 2020, Control Namba 9910817687235.**

## TANGAZO LA KUPOTELEWA NA PASIPOTI YA KUSAFIRIA.



**Khalfan Nassor Abdallah**
Anatangaza kupotelewa na Pasipoti ya kusafiria namba TAE O87990 ambayo aliipata kupitia Ofisi ya uhamiaji makao bara makuu (PCO, Dar es salaam).
Kwa yeyote atakae iona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Khalfan Nassor Abdallah kwa simu namba 0765796146.
**RB NAMBA: NGR/RB/4215/2020.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**LEAH WILFREDY MACHA**
Anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.2028/026 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary MARINGENI mwaka 2012,yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa MAG/RB/1398/19**

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz
au piga Simu: 0782253676

**MWAMBA AUCTION MART AND RECOVERIES**
P.O.BOX 429 DODOMA – TANZANIA
OFFICE LOCATION: CCM REGIONAL BUILDING ROOM No. 9
0715170553 / 0756011439

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Tunautangazia umma kuwa, kwa amri ya Mahakama Kuu ya Tanzania-Dodoma nitauza kwa mnada wa hadhara kiwanja chenye vipimo (coordinates) **1-LVR 841,LVR 842, LVR 84362-LVR 843, LVR 604, LVR 603, LVR93-LVR9, LVR 602, LVR 5,4-LVR 5, LVR 141, LVR 859** kilichopo mtaa wa **MIYUJI PROPER kata ya MIYUJI JIJI LA DODOMA mali ya IBRAHIM JUMA KASIKA** anayedaiwa na **RASHID SEIF ABEID KILAMA** ikiwa ni utekelezaji nambari 7 wa mwaka 2020. Mnada utafanyika katika eneo hilo na litauzwa kama lilivyo. Mnada utafanyika siku ya Jumatano ya tarehe **11 Novemba 2020** saa tatu na nusu asubuhi.

Dalali wa Mahakama ndiye mwendesha mnada, hivyo ndiye mwenye kupiga nyundo ya mwisho. Mteja mwenye bei ya juu ndiye atakayetangazwa mshindi.

**Kwa mawasiliano piga 0735170553 na 0715170553 (Dalali wa Mahakama).**

## KUPOTEA KWA KADI YA TREKTA

**Eden Samson Matoi** anatangaza kupotelewa na kadi ya trekta aina ya marcey ferguson yenye namba za usajili T 298 AHA. yoyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**taarifa ya polisi: kil/rom/rb/777541/2020.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FLORA JACOB MAKONGORO**
Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA RUSH yenye namba za usajill T 929 CBG chasis namba J200E0024087 yeyote atakayeiona atoe tarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa DAR/BUG/RB/780076/2020**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI PICHANI

# SHEREHE ZA KUAPISHWA RAIS DK. JOHN MAGUFULI



Rais Dk. John Magufuli akiwapungia mkono wananchi waliohudhuria sherehe za uapisho wake, alipowasili katika Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**



Rais Dk. John Magufuli akikagua gwaride la heshima lililoandaliwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), kabla ya kuapishwa jana. **PICHA: IKULU**



Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma (kulia), akimkabidhi katiba ya nchi, Rais John Magufuli, baada ya kumwapisha kuwa Rais wa Tanzania, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma (kulia), akimwapisha Samia Suluhu Hassan kuwa Makamu wa Rais wa Tanzania, wakati wa sherehe hizo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Kikosi cha Askari wa Makomando, kikipita kwa ukakamavu mbele ya Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Rais John Magufuli, baada ya kuapishwa. **PICHA: IKULU**



Baadhi ya viongozi wa siasa na kiserikali wakishiriki sherehe hizo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**




# SOLSKJAER
## ASEMA AHOFII KUFUKUZWA

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amesisitiza "amebakia imara" licha ya uvumi kuzagaa kuhusu hatima yake.

Solskjaer yupo kwenye presha kubwa pale Old Trafford baada ya United kuchapwa mabao 2-1 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Istanbul Basaksehir.

Raia huyo wa Norway alikataa kuzungumza kuhusu majaliwa yake, lakini akasema amebakia imara sana.

"Nimekataa kuzungumza kuhusu hilo. Bila shaka ni mapema mno," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari.

"Shutuma zipo mara zote, unatakiwa kubakia imara na nimeajiriwa na klabu kufanya kazi na nafanya kadiri ya uwezo wangu pamoja na wenzangu."

Ikiwa nafasi ya 15 kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, United imekumbana na vipigo mfululizo kuelekea kwenye mchezo dhidi ya Everton, Jumamosi.

Solskjaer amesema kufungwa kunaumiza, na hasa kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya uliopita.

"Bila shaka matokeo ya mechi mbili zilizopita yaumiza tumbo kwa uhakika kabisa," alisema.

"Kitu pekee ninachojua ni kuendelea kuwa na matumini na wachezaji wakati huu tukielekea kwenye mchezo dhidi ya Everton, kwa sababu najua utakuwa mgumu."



# KOEMAN: TER STEGEN AMEIBEBA BARCA

**KIEV, Ukraine**

RONALD Koeman ameshukuru "kiwango cha kuvutia" cha Marc-Andre ter Stegen wakati Barcelona wakipata ushindi mwembamba wa mabao 2-1 dhidi ya Dynamo Kiev na kukubali kwamba kikosi chake kina kazi kubwa ya kufanya.

Miamba hao wa Katalunya walishinda mchezo huo wa tatu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya katika Kundi G, wakati Lionel Messi akifunga kwa penalti dakika ya tano na Gerard Pique akifunga kwa kichwa kipindi cha pili.

Hata hivyo, Barca ilihitaji Ter Stegen aokoe hatari sita langoni mwao dhidi ya Dynamo ili kujihakikishia ushindi huo.

"Amethibitisha kwamba ni golikipa bora kwa upande wetu," alisema Koeman akiiambia Movistar baaada ya mchezo huo.

"Amekuwa akijifua vizuri zaidi na sisi na mmeliona hilo kwa mchezo wa leo (juzi).

"Tulianza mchezo vizuri kwa kupata bao la haraka na kuongoza kwa 1-0, lakini tukashindwa kupata bao la pili na baadaye tukapoteza utawala wa mchezo.

"Shukrani kwa Marc, ambaye alicheza kwa kiwango cha kuvutia zaidi, na tukaweza kupata ushindi huo."

# TUCHEL: SIKO HATARINI PSG

**PARIS, Ufaransa**

THOMAS Tuchel hajihisi kazi yake ya ukocha pale Paris Saint-Germain ipo hatarini baada ya kikosi chake kufungwa magoli 2-1 na RB Leipzig kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

PSG ilianza kwa kupata bao la kuongoza katika dimba la Red Bull Arena kupitia kwa Angel Di Maria, lakini wakajikuta kwenye wakati mgumu baada ya nyota wake huyo raia wa Argentina kukosa penalti.

Kiungo wa zamani wa PSG, Christopher Nkunku, alisawazisha na penalti ya Emil Forsberg ikawapa ushindi, huku Idrissa Gueye na Presnel Kimpembe wakitolewa nje kwa kadi nyekundu.



Ikiwa imefungwa mfululizo kwenye michuano hiyo katika Kundi H, PSG ina pointi tatu nyuma ya vinara Manchester United na Leipzig, ikiwa kwenye wakati mgumu wa kufuzu hatua ya mtoano.

Lakini Tuchel alikataa kuona hatari ya kibarua chake na kusema anaamini mambo yatabadilika tu kwa kikosi hicho.

Aliambia RMC: "Ilikuwa ngumu, lakini pengine ni kutokana na makosa yetu, kwa sababu hatukufunga bao la pili na tukafanya kosa la kutoa penalti.

"Halafu mambo yakawa magumu zaidi, tukampoteza mchezaji, kulikuwa na maamuzi mengi ya kutuumiza sisi."

## HABARI MICHEZO



# KIWANGO CHA WERNER CHAMFURAHISHA LAMPARD

**LONDON, England**

FRANK Lampard alifurahishwa na namna Timo Werner alivyozoea haraka mazingira pale Chelsea baada ya mshambuliaji huyo kufunga mara mbili kwa penalti wakati wakishinda 3-0 dhidi ya Rennes kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Werner alifunga bao la kwanza dakika ya 10 baada ya kudondoshwa na Dalbert, ambaye baadaye alimchezea tena rafu na kupewa kadi ya pili ya njano iliyozaa nyekundu na kumruhusu nyota huyo mwenye umri wa miaka 24 kufunga tena kwa penalti bao la pili.

Tammy Abraham aliongeza bao la tatu na kuwawezesha Chelsea kufikisha pointi saba sawa na Sevilla kwenye Kundi E.

Penalti hizo mbili zilimfanya Werner kufikisha mabao saba katika mashindano yote tangu atue hapo kutokea RB Leipzig kwa ada iliyoripotiwa kuwa pauni milioni 47.5.

Lampard amesema kwamba, Werner ameonyesha kuzoea haraka mazingira na amekuwa akiimarika siku hadi siku na amekuwa na mwanzo wa kuvutia.

"Kwamba ameweza kuonyesha kuwa yuko fiti zaidi kwenye mazoezi akiwa na sisi," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Amezoea haraka mazingira na imekuwa rahisi kwake kucheza kwa upatina mzuri na wenzake.

"Yupo kwenye kiwango cha kuvutia sana. Naamini ataendelea kuimarika siku hadi siku."



# ZAMALEK YATINGA FAINALI CAF

**CAIRO, Misri**

ZAMALEK imetinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Raja Casablanca na sasa wanajiandaa kucheza na Al Ahly kuwania taji hilo kubwa zaidi kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Baada ya ushindi wa mchezo wa kwanza wa 1-0, Achraf Bencharki aliwafungia bao la kwanza mabingwa hao mara tano wa mashindano hayo, kabla ya Mostafa Mohamed kufunga mara mbili na kuwapa ushindi huo.

Ben Malango alifunga la kufutia machozi kwa Raja Casablanca.

Ushindi huo wa Zamalek wa 3-1 maana yake sasa imetinga fainali kwa ushindi wa uwiano wa mabao 4-1.

Mchezo huo wa pili wa nusu fainali uliahirishwa mara mbili kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Sasa Zamalek inajiandaa kwa fainali itakayopigwa kwenye dimba la Borg El Arab jijini Alexandria nchini Misri Novemba 27, dhidi ya Al Ahly ambao iliwatoa Wydad Casablanca kwenye nusu fainali.

***



# INGS AFANYIWA UPASUAJI WA GOTI

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa Southampton, Danny Ings jana, Alhamisi, alifanyiwa operesheni ya goti na anaweza kuwa nje ya dimba kwa wiki sita, kwa mujibu wa Kocha Ralph Hasenhuttl.

Ings aliumia goti wakati Southampton ikiibuka na ushindi wa 4-3 dhidi ya Aston Villa Jumapili na alithibitika kwamba nyota huyo wa kimataifa wa England anahitaji kufanyiwa upasuaji.

Kwa wakati huu inaonekana anaweza kuwa nje ya dimba kwa wiki nne hadi sita," alisema Hasenhuttl, kuelekea kwenye mchezo wa leo Ijumaa dhidi ya Newcastle kwenye Ligi Kuu England.

"Atafanyiwa upasuaji leo (jana). Ni habari mbaya kwetu kwa sababu atakuwa nje kwa muda mrefu."

Ings alilazimika kutolewa nje ya dimba dakika ya 85 pale kwenye dimba la Villa Park baada ya kufunga bao lake la tano msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 aliumia baada ya kugongana na Trezeguet aliyeingia kwenye kikosi cha Villa akitokea benchi.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MORATA AFUNGUKA KUHUSU UBORA WAKE

Mshambuliaji huyo aweka wazi kuwa sasa amekamilika na anafurahia uzoefu ambao ameupata...

**BUDAPEST, Hungary**

ALVARO Morata anahisi "amekamilika zaidi" wakati akizungumzia furaha yake kwenye kikosi cha Juventus baada ya kuendelea kuwa kwenye kiwango bora cha kufunga.

Morata alifunga mabao mawili wakati Juve wakiifumua Ferencvaros mabao 4-1 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumatano.

Mshambuliaji huyo amefunga mabao sita katika mechi tano zilizopita za ugenini kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Morata, ambaye ana mabao sita katika mechi saba msimu huu, amesema ana furaha zaidi wakati wake huu wa kipindi cha pili cha kucheza kwa klabu hiyo ya Turin.

"Tulikuwa na furaha na pointi tatu tulizopata, ni muhimu kwamba tumeshinda mechi mbili baada ya muda wa kuzoea, lakini tunajua bado tunaweza kuimarika zaidi," alisema akinukuliwa na tovuti ya klabu hiyo.

"Kama tukiendelea kama hivi, tunaweza kwenda mbali zaidi. Najihisi vizuri, nimekamilika zaidi, sasa nina uzoefu mkubwa katika kipindi changu cha uchezaji na kimenisaidia mimi kukua.

"Hicho ndio kitu nilichokuwa nahitaji zaidi, najihisi kama bingwa wa kiwango cha juu zaidi kwa sasa."

Paulo Dybala pia alifunga kwenye ushindi huo na Lasha Dvali akajifunga na kuwazawadia Juve bao la nne, huku Franck Boli akafunga la kufutia machozi.

Miamba hao wa Ligi Kuu Italia, Serie A, wameshinda mechi 10 kati ya 14 za ugenini kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya makundi, zikiwamo nne mfululizo.

Mlinzi wa Juve, Giorgio Chiellini, ameshauri wachezaji wenzake kuendelea kuimarika zaidi baada ya kupata pointi sita katika Kundi lao la G.

"Tumeridhishwa na matokeo, lakini tungeweza kufanya zaidi," alisema.

Kwenye Ligi Kuu Juve inashika nafasi ya tatu katika msimamo na watacheza ugenini dhidi ya Lazio, Jumapili.

## KWA UFUPI

**BAYERN YAMTAKA ALABA**
MWENYEKITI wa Bayern Munich, Karl-Heinz Rummenigge amesema anataka mlinzi wa Austria, David Alaba abaki kwenye klabu hiyo, lakini uamuzi wa mwisho uko mikononi kwa mchezaji huyo ambaye ana umri wa miaka 28. ***(Bild)***

**ALABA AINGIA SOKONI**
KLABU ya Real Madrid inataka kumsajili, David Alaba ambaye ana umri wa miaka 28 mara tu mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu.***(Diario)***

**HAALAND YUKO HURU**
MSHAMBULIAJI wa Norway, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 20, hana kipengele cha uhamisho kwenye mkataba wake, kwa mujibu Mtendaji Mkuu wa Borussua Dortmund, Hans-Joachim Watzke. ***(Bild)***

**BARCA YAMTAKA NDOMBELE**
KLABU ya Barcelona inaweza kujitosa kuwania kumsajili kiungo wa Tottenham na Ufaransa, Tanguy Ndombele mwenye umri wa miaka 23 wakati wa dirisha lijalo la usajili. ***(Fabrizio Romano)***

**SALIBA NJIA MOJA**
KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amesema kuwa beki wa kati Mfaransa, William Saliba anaweza kuondoka kwa mkopo wakati wa dirisha dogo la Januari mwakani. ***(Mail)***

**ALVAREZ AITAMANI CITY**
MLINZI wa Ajax, Edson Alvarez mwenye umri wa miaka 23, amebainisha shauku yake ya kutaka kujiunga na Manchester City siku moja. ***(Voetbalzone)***

**UNITED ILIMKOSA DIABY**
MANCHESTER United ilishindwa kumsajili winga Bayer Leverkusen, Moussa Diaby mwenye umri wa miaka 21, wakati wa dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto lililopita. ***(Bild)***

**ARTETA AMKATAA ELNENY**
KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta hayuko tayari kuzungumzia kuhusu kuongeza mkataba kwa ajili ya kiungo wa kati wa Misri, Mohamed Elneny mwenye umri wa miaka 28, na ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu. ***(Goal)***

**MADRID, RAMOS WATETA**
REAL Madrid imeanza mazungumzo ya kumpa mkataba mpya nahodha wake, Sergio Ramos mwenye umri wa miaka 34. ***(ESPN)***

**AGBONLAHOR KUULA**
MSHAMBULIAJI wa zamani wa Aston Villa, Gabriel Agbonlahor amesema mkataba mpya wa kiungo wa kati wa Scotland, John McGinn mwenye umri wa miaka 26, utakaotangaza na klabu hiyo utakuwa na ofa kubwa. ***(Football Insider)***

**LEEDS YAITA WAWEKEZAJI**
MMILIKI wa Leeds United, Andrea Radrizzani amesema amefungua milango kwa wanaotaka kuingia ubia katika kuiongoza klabu hiyo kama ilivyo katika kampuni za Red Bull na City Football Group, ambazo ni kampuni mama za Manchester City. ***(Yorkshire Evening Post)***

**GREENWOOD KUREJEA ENGLAND**
MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Mason Greenwood, 19, alitarajiwa kurejea katika kikosi cha Timu ya Taifa ya England hapo jana. ***(Guardian)***



HABARI MICHEZO

# SVEN AJIPANGA KURUDI KILELENI LIGI KUU BARA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa mabingwa watetezi Simba, Sven Vandenbroeck, amesema mipango yake ni kuhakikisha wanapambana na kupata ushindi katika mechi tatu mfululizo ili kurejea katika uongozi kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mechi mojawapo ambayo Sven anahitaji kushinda ni dhidi ya watani wa jadi, Yanga itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili, Sven alisema baada ya kupoteza pointi katika michezo yake miwili aliweka mikakati ya kushinda kila mechi ulioko mbele yake na tayari amepata matokeo mazuri dhidi ya Mwadui na Kagera Sugar.

Sven alisema sasa wanaendelea na maandalizi kwa ajili ya kutafuta pointi tatu dhidi ya Yanga baada ya hapo atasaka ushindi mwingine katika mechi nyingine zitakazofuata.

"Malengo yetu ni kutetea ubingwa, lakini lazima tupambane kutafuta matokeo mazuri kwa kila mechi zetu bila kujali tunacheza na timu gani, wachezaji wangu wanajua hilo na kila utakayempa nafasi anaonyesha kiwango kizuri."

"Leo (juzi), nimewapa nafasi wachezaji ambao wametoka katika majeruhi, Chris Mugalu na Ame Ibrahim wamefanya kazi nzuri," alisema Sven.

Kocha huyo alisema baada ya mechi ya juzi dhidi ya Kagera Sugar na kuibuka na ushindi wa mabao 2-0, mchezo huo ameufanya ni sehemu ya maandalizi ya kuikabili Yanga.

"Tunaenda kujipanga kwa mechi zetu zijazo, hivi sasa tunajiandaa dhidi ya Yanga, tunafanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika mechi zilizopita, tunataka kuingia tukiwa imara na kwenye ubora," alisema Sven.

Kuhusu Mugalu alisema amerejea kikosini baada ya kupona majeraha ya nyoga na ana imani mechi ijayo atakuwa miongoni mwa wachezaji watakakuwapo katika mipango yake.

"Kwa mujibu wa taarifa kutoka kwa daktari wetu wa timu, tutawakosa wachezaji wawili Meddie Kagere pamoja na Gerson Fraga ambao wanamajeruhi ya muda mrefu," aliongeza kocha huyo.

Alieleza malengo yake ni kuona timu hiyo inarejea katika nafasi ya juu kwenye msimamo wa ligi kabla ya kuanza kampeni ya kupeperusha bendera ya nchi kwenye mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.



Wachezaji wa KMC FC wakiwasili jijini Dar es Salaam, jana, wakitokea Mwanza ambapo walienda kucheza mechi tatu za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu unaoendelea. Kikosi hicho kimevuna pointi nne katika michezo hiyo mitatu iliyochezwa Kanda ya Ziwa. **PICHA: MTANDAO**

## Wanariadha, baiskeli kuchuana Des. 9

**Na Saada Akida**

MASHINDANO ya riadha na mbio za baiskeli ya kusherehekea Uhuru wa Tanzania yamepangwa kufanyika Desemba 9, mwaka huu jijini Dar es Salaam imeelezwa.

Akizungumza jijini jana, Mkurugenzi wa Kampuni ya Uhuru Sports Agency, Leena Kapadia, alisema mashindano hayo yatashirikisha wanariadha wanawake na wanaume kwenye mbio za nusu marathon (kilomita 21), huku kwa upande wa waendesha baiskeli watashindana mbio za kilomita 42.

Kapadia alisema mbali ya mashindano hayo, pia kutakuwa na mbio za kilomita tano ambazo washiriki wanaweza kukimbia au kutembea na zimeandaliwa maalum kwa watu wazima, vijana huku watoto watachuana katika mbio za kilomita 10.

Alisema usajili kwa wanamichezo wanaotaka kushiriki mashindano hayo utafanyika Novemba 15, mwaka huu na kamati yao kwa sasa inatafuta wadhamini kwa ajili ya kufanikisha michuano hiyo.

"Haya ni mashindano ya kwanza ya kusherehekea Uhuru wa Tanzania kwa kushirikisha wanariadha na waendesha baiskeli. Kampuni yetu imesajiliwa na Baraza la Michezo la Tanzania (BMT), tunatarajia kuandaa mbio zitakazovutia na zenye ushindani mkubwa," alisema Kapadia.

Kiongozi huyo alisema wanatarajia kuona viongozi wa kampuni za umma, binafsi, mabalozi na taasisi mbalimbali zinajitokeza kushiriki katika mbio hizi.

Alisema wanatarajia wanamichezo wasiopungua 3,500 watashiriki katika mashindano hayo, ambapo miongoni mwao ni wanariadha nyota wa ndani ya nchi.

Kapadia alisema mashindano hayo pia yana lengo la kuendeleza mchezo wa riadha na baiskeli hapa nchini.

## Viingilio Mwakinyo, Jose Paz hadharani

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI maandalizi ya pambano kati ya bondia, Hassan Mwakinyo dhidi ya Jose Carlos Paz kutoka Argentina yakiwa katika hatua za mwisho, kiingilio cha chini cha kushuhudia mtanange huo kimetajwa kuwa ni Sh. 150,000.

Pambano hilo la kuwania ubingwa wa Mabara wa WBF na IBA wa uzito wa Super-Welter litafanyika Novemba 13, mwaka huu Next Door Arena ulioko Oysterbay jijini, Dar es Salaam.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Jackson Group Sports, Kelvin Twissa, alisema pia kutakuwa na meza ya watu 10 ambayo itauzwa kwa Sh. milioni tatu na wadau watakaonunua tiketi hizo watapata huduma mbalimbali.

Twissa alisema katika kuwarahisishia wadau kupata huduma hiyo bila usumbufu, wanatarajia kuuza tiketi za pambano hilo kwa njia ya mtandao kupitia Kampuni za Nilipe na Selcom.

Alisema katika kuhakikisha mikanda hiyo miwili inabakia nchini, Mwakinyo ameamua kuweka kambi katika eneo la Magoroto, Muheza akiwa chini ya kocha wake, Hamis Mwakinyo.

Alitaja mapambano mengine ya utangulizi yatakayofanyika siku hiyo ni kati ya bondia nyota wa kike, Zulfa Macho dhidi ya Alice Mbewe kutoka Zambia wakati Hussein Itaba atazichapa na Alex Kabangu katika uzito wa Super Middle huku Mkenya, Fatuma Zarika atazidunda na Patience Mastara wa Zimbabwe.

## Kahama Marathon kufanyika Jumapili

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WANARIADHA zaidi ya 300 wanatarajiwa kushiriki katika mbio za Kahama 'Kahama Marathon 2020' zitakazofanyika Jumapili katika halmashauri ya mjini hapa.

Kahama Marathon inafanyika kwa mara ya kwanza na inatarajia kushirikisha wanariadha wanaume na wanawake kutoka kada mbalimbali hapa nchini.

Akizungumza mkoani hapa jana, Balozi wa Keke Events Agency, Caroline Joseph alisema maandalizi kwa ajili ya mbio hizo yamekamilika na anatoa wito kwa wakazi wa Kahama kujitokeza kushiriki katika mashindano hayo.

Mratibu huyo alisema malengo yao ni kupata washiriki zaidi ya 500, lakini mpaka sasa tayari wanariadha 350 wamethibitisha kushiriki mbio hizo kutoka mikoa ya Mara, Singida, Arusha, Geita, Mbeya, Dodoma, Dar es Salaam, Shinyanga na Mwanza.

Alisema mapato yatakayopatikana katika tamasha hilo ambalo kauli mbiu yake ni "Okoa vifo vya kinamama wajawazito na watoto" yatapelekwa kusaidia wanawake wajawazito na watoto kwenye Hospitali ya Mji wa Kahama.

Naye Ofisa Michezo wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, Lupola Mkomwa, aliwapongeza waandaaji wa mbio hizo na kueleza zitasaidia kuibua vipaji na kupunguza tatizo la ajira kupitia mchezo huo wa riadha.

Mkurugenzi wa Keke Event Agency, Sia Kimambo, alisema wanatumia fursa ya mbio hizo kuitangaza Wilaya ya Kahama na wanaamini itasaidia kukua kiuchumi.

Kimambo alisema mbio hizo zinafanyika kwa kushirikiana na Kampuni ya Bia Tanzania (TBL), Jambo Group, Keke Bridal and Event, Stockholm Carwash, Hawk Motors, Emirates Aluminum, Jema Africa, Nzengo Bar Grill, Shule ya Rocken Hill na Lakezone Runners.

Michezo
Ijumaa Novemba 6, 2020
Nipashe



MORATA AFUNGUKA KUHUSU UBORA WAKE HABARI UK 22



Beki wa Simba, Mohamed Hussein (kulia), akijiandaa kumtoka winga wa Kagera Sugar, Ally Ramadhani katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Dar es Salaam juzi. Simba ilishinda mabao 2-0 **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TAIFA STARS KAMBINI LEO

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kuonekana kuwa na msimu mzuri, mshambuliaji wa JKT Tanzania, Adam Adam amejumuishwa katika kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars), kitakachoingia kambini leo kujiandaa na mechi ya kusaka tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Afrika dhidi ya Tunisia.

Kikosi hicho cha Stars kilichoko chini ya Mrundi Etienne Ndayiragije, kitaondoka nchini Jumapili na kuelekea Tunis kwa ajili ya mchezo huo wa kwanza utakaochezwa Novemba 13, mwaka huu.

Wachezaji wengine wa Stars walioitwa kujiandaa na mchezo huo ni pamoja na Juma Kaseja, Metacha Mnata, Aishi Manula, David Mapigano, Shomari Kapombe, Deus Kaseke, Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr', Bryson David, Bakari Mwamnyeto, Abdallah Kheri na Abdallah Shaibu 'Ninja'.

Nyota wengine ni Jonas Mkude, Himid Mao, Erasto Nyoni, Simon Msuva, Ditram Nchimbi, Feusal Salum 'Fei Toto', Ally Msengi, Mbwana Samatta, John Bocco, Mzamiru Yassin, Iddi Suleiman 'Nado', Thomas Ulimwengu, Farid Mussa, Said Ndemla, Salum Aboubakar 'Sure Boy' na Adam Adam.

Baada ya mchezo huo wa kwanza, Stars itarejea nchini na kuwakaribisha Waarabu hao wa Tunisia Novemba 17, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.

Mechi nyingine za Kundi J katika mashindano hayo yanayosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), zitakuwa ni kati ya Libya dhidi ya Equatorial Guinea.

# TALIB AZICHAMBUA SIMBA, YANGA

## ●●●Lakini aipa nafasi ya ushindi Simba, huku Chama akiwa na hatihati kushuka dimbani...

**Na Somoe Ng'itu**

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa Simba, Talib Hilal, amesema anaipa nafasi timu yake hiyo ya zamani kuibuka na ushindi katika mechi dhidi ya watani wao wa jadi, Yanga itakayochezwa kesho endapo mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Bara wataonyesha kiwango chao halisi katika mchezo huo.

Simba itashuka katika mchezo huo ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 4-1, walioupata kwenye mechi ya hatua ya nusu fainali ya Kombe la FA, lakini ikivuna alama moja tu katika Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya watani zao msimu uliopita.

Akizungumza na Nipashe jana, Talib, alisema Simba ina wachezaji wenye kiwango kizuri zaidi katika kila idara ukilinganisha na watani zao, lakini kukaa kwa muda mrefu pamoja kunawafanya wafahamiane zaidi.

Talib alisema pia safu ya ushambuliaji ya Simba ina 'makali' zaidi na kurejea kwa straika Mzambia Chriss Mugalu, aliyekuwa majeruhi kunakiongezea nguvu kikosi hicho kinachofundishwa na Sven Vandenbroeck ambaye anashirikiana na nahodha wa zamani wa timu hiyo, Suleiman Matola.

"Simba ni wazuri karibu kila nafasi, ninawapa nafasi ya kushinda kama watacheza mpira wao tunaoujua, kurudi kwa Mugalu kutasaidia sana kuongeza nguvu pale mbele, ni mchezaji mhangaikaji," alisema Talib.

Alisema Simba imekuwa ikitengeneza nafasi nyingi za kufunga lakini haizitumii vyema na kuwafanya wapoteze ushindi katika mechi mbili dhidi ya Tanzania Prisons na Ruvu Shooting.

"Simba tunatengeneza nafasi nyingi lakini hatufungi, hili linatakiwa kufanyiwa kazi zaidi, ushindani ni mkubwa na hasa kutoka kwa Azam FC," Talib alisema.

Alisema pia Yanga ina timu nzuri hasa katika idara ya viungo, lakini pia washambuliaji wake hawatakiwi 'kubezwa'.

Aliongeza wachezaji wa Yanga wanacheza mpira wa kasi na mfumo huo umewasaidia kuwapa matokeo mazuri kwenye mechi zilizopita na kuifanya kuwa timu pekee hadi sasa ambayo haijapoteza mchezo.

"Yanga ina timu nzuri, viungo na safu yao ya mbele si ya kuachwa, wachezaji wake wanacheza kwa kasi, Simba inatakiwa iwe makini kwa sababu Yanga wanategemea sana magoli ya kona, mabeki wetu (Simba), wanatakiwa kuongeza umakini," aliongeza kocha huyo.

Alisema pia kila timu imekuwa na 'kiu' ya kuonyesha ubora wake lakini anaamini kupitia mchezo huo timu mojawapo itarahisisha safari yake ya kuwania ubingwa wa msimu huu.

Yanga ndio mwenyeji wa mchezo huo na ataikaribisha Simba akiwa na kumbukumbu ya kutoka sare ya bila kufungana na Gwambina FC ya Mwanza wakati mabingwa watetezi wenyewe walipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Kagera Sugar.

Kikosi cha Cedric Kaze, Yanga kina pointi 23 wakati wawakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu, Simba ina pointi 19, kila timu ikiwa imecheza mechi tisa.

Wakati huo huo, taarifa kutoka katika kambi ya Simba zinaeleza kiungo, Clatous Chama huenda akaukosa mchezo wa kesho kutokana na kupata matatizo.

Taarifa zaidi zinasema hadi jana jioni, Sven amemwondoa Chama katika mipango yake kuelekea mchezo huo wa raundi ya 10 wa Ligi Kuu Bara.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002